Njuricheke ilikuwa na role mhimu sana hata ingawa hakuna pahali hapakosi kasoro. Njuricheke ilifanya kitu muhimu hapa pale zamani. Bwana Commissioner, vile unionavya mimi ni member wa Njuricheke na kwa hivyo wale wanataja mambo ingine mbaya mbaya ya Njuricheke ni wale hawajui. Njuricheke ilifanya kazi mzuri kwa sababu ndiyo ilikuwa ikiamua makesi kabisa ata kabla ya serikali kuundwa ata kabla ya mkoloni kuingia hapa kwa hivyo wale wazee waheshimiwe yale mambo ambayo ni mhimu kwao watakiwa kwa uamuzi wapewe hiyo jukumu na watambuliwe kabisa kama chombo mhimu na sisi wameru. Kwa hayo machache ni asante sana Bwana Commissioner.

Com. Zein: Asante sana Councilor. Councillor tafadhali andika jina lako kwenye register kwamba umetoa maoni yako. Sasa ningependa kumualika Commissioner Mwenzangu Mzee Ratanya aendelea na shuguli hizi za kuongoza kuchukuwa maoni. Naoni mzee mmoja anainua mkono tunafuata orodha ya majina ya watu waliojiandikisha mzee wangu. Umeandikwa basi suburi utafikiwa. Bwana Ratanya.

Com. Ratanya: (talking in Kimeru). Kwa hivyo asante Bwana Zein sasa utapumzika dakika chache na mimi nitachukuwa sasa. Thank you very much. Umefanya hii yote ni wewe umekamilisha pale niliachia asante. Kabila hatujaendelea wananchi ninaangalia hapa nimeona Mheshimiwa wetu wa sasa Maore alifika hapa sikukua nimefika. Salaam sana Bwana Mheshimiwa, Hon. Moare asante sana, nakusalimia. Hukukuwa hapa wakati nilipokuwa hapa. Na hapo hapo ninaona Mheshimiwa wetu ambaye alikuwa mbeleni hapo kidogo kabla ya Maore former MP Bwana Joseph Muturia yuko hapa, so we recognize your presence Bwana Joseph Muturia. So Mheshimiwa umekaribishwa.

Na kwa hivyo kutoka hapo sasa tutaendelea vile yule Commissioner mwenzangu ameacha, pale ameachia is number --- Mutiri Julius. Is Julius Mutiri is he around? Julius yuko. Okay tuende kwa mwingine ni Francis Meme. Endelea Francis.

Francis Meme: Mimi yale maneno nitaweza kuzungumzia ni maneno ya hospital watu siku hizi hawapati dawa. Kwa Jina ni Francis Meme.

Upande wa hospital zile za serikali watu hawapati huduma sawa sawa. Mama anakwenda huko na mtoto anaambiwa achukuwe receipt ili apate dawa, akaandikiwa akaambiwa aende chemist, anarudi na mtoto bila kupata matibabu na watoto wanakufia nyumbani. Wale watu hawana idini ya kuuza madawa hapa ndiyo wanauza madawa. Watu wanapelekwa hata maternity huko wanakwisha kwa ugonjwa na ni daktari ambaye amehitimu.

Serikali yetu iruhusu kila clinic ifunguliwe kila mahali kwa madaktari (inaudible) watu wawe wakipata huduma sawa sawa kwa matibabu na hospitali kila Division serikali ifikirie iwe na hospital kuu ya watu (inaudible) na kupata matibabu. Hiyo ndiyo maoni yangu kama ni wasichana nao wazazi wasiruhusu wasichana kuolewa bila kijana kupelekwa kwa daktari kufanyiwa uchunguzi kama ako na ukimwi au ---- halafu ndiyo wazazi waruhusu watoto wapalekwe kwa hospital hiyo nataka ingizwe kwa Katiba. Mtoto awe akipata matibabu yule wa kijana na yule wa msichana, ili waruhusiwe kufunga ndoa, nataka hiyo iingie kwa Katiba ili tuweze kuzuia ukimwi. Asante hayo ndiyo maoni yangu.

Com. Ratanya: Okay asante sana Julius. Sasa nikiangalia naona kuna Richard Maore Mauka Hon. MP wetu wa sasa hebu endelea.

Hon. Richard Mauka: Wana Commissioners wote wawili, kwanzia naomba msamaha kwa kuja nikiwa nimechelewa lakini ningependa kueleza kwamba wajibu wangu sana siyo kutoa maoni hapa kwa sababu sisi tutakuwa na foruma nyingine nyingi za kutoa maoni. Kwanza itakuwa ile inaitwa National Constitutional Conference, baadaye ikamaliza hapo itatukuta huko Bungeni kwa hivyo ingekuwa selfish kwa Kiingereza ama ubinafusi kwa Kiswahili sanifu, Kuchukuwa nafasi ambayo nyinyi mngochukuwa wenyewe kueleza maoni yenu kwa Katiba, na mimi nitakaa hapa nianze kueleza yote yale nafikiria na nyinyi mkose nafasi ya leo. Kwa hivyo ningetaka tu kutaja machache kwa ubinafusi yale ningefikiria ni mhimu yawe yanazungumziwa. Ukiangalia ile Katiba tumekuwa nayo miaka karibu arobaine kwanzia ningependa kueleza haikukuwa na kasoro ama itilafu nyingi isipokuwa tamaa ya vyongozi kupenda kubalidisha mahali walikuwa wanataka wakiamka asubuhi wanafikiria hii inawasumbua wanatoa hiyo wakienda kulala usiku wakiona hii inawasumbua wanatoa mpaka wakiaribu.

Kwa hivyo kwenye zile zura ziko kwenya Katiba yetu ningependa tu kutaja machache.

The old Constitution has 11 chapters. Kutoka the 11 the last two were not much of a story. Ya kwanza ni utangulizi, ya pili ni kueleza maneno ya Raisi na Makamu wa Raisi na halafu na Mawaziri na Baraza la Mawaziri. Hapo ningependa kupendekeza Bwana ma-Commissioner ni vizuri wakenya wanapoongea juu ya neno Provinces, mahali imetajwa kwamba ukuu wa Raisi

lazima uwe na asilimia 25 kwa mikoa mitano, hiyo si mbaya. Halafu iongezwe pia yule atakuwa Raisi awe juu ya hiyo asili mia 25, kwa mikoa mitano awe na asili 51. Hiyo ndiyo ile njia ya pekee unaweza kujua yule anapendwa na wakenya wote. Ikiwa haufiki hapo ufanye ile inaitwa run—off, sababu ndiyo kwenye hiyo run-off utapata yule ambaye anapendwa zaidi.

Pili, hapa hapo kwa Provinces kwa Kingereza wanasema siyo Constitution entity. There is no where in the Constitution where we talk of the Provinces. Kama zimewekwa hii ni najua ni kinyume cha Katiba lakini hiyo mahakama ya siku hizi hata ukipeleka huko you will be wasting your money and your time, ndiyo tunasema kwenye huu mjadala wa Katiba, Provinces ziwe defined katika Katiba. Baada ya kuwa defined ndiyo inaweza kutumika as a Constitution entity.

Hiyo nyingine kidogo hapo hapo tu kwenye maneno la baraza ya mawaziri kuna haya maneno- anaitwa Assistant Minister. Wengi wanajua Mheshimiwa Muturi alipokuwa Assistant Minister wa transport and Communication, hakukuwa anauliza maswali bungeni na hakuweza kusema barabara ikuje hapa haraka, kwa sababu definition ya mawaziri, assistant Ministers, hawakuwi na zile Executive powers. Ndiyo tunaweza kupendekeza kwamba Assistant Ministers wabadilishwe wawe Deputy Ministers, ili waweze kwa-access hata cabinet memorandums. Unaweza kuwa Assistant kwa miaka zaidi ya ishirini, kama akina Moody Awouri ama Mathias Keya lakini hujawai kuona cabinet paper hata siku moja. Kwa hivyo ni vizuri waweze kupewa uwezo. Ukiwa Assistant Minister uwe una uwezo kama yule unaitwa Minister mwenyewe.

Baada ya kumaliza hapo maneno ya hii President najua hii maneno ya President ndiyo imeleta the all debate maneno ya Constitution katika nchi hii. Kuwe na uwezo ambayo President akiwa amefanya dhambi akiwa kwa office asiwe anafunikiwa na kitu tunaitwa above the law.

Above the law means the most crucade of the criminals. Ipangwe awe anakuwa impeached if he is found with the offences of abusing public office kwa hivyo iwe inaweza kuwa mhimu pia.

Halafu kwa haraka maneno ya Parliamentary boundaries. Tutumie idadi ya watu as the main measurement wakati unataka kupanga kubadilisha mipaka. Si vizuri kukuta Constituency kama hii iko na wapiga kura zaidi ya elfu arobaine ukute ingine chini kidogo ukitoka hapa ukienda Constituency unatoka pande unakuta iko na elfu mbili, tatu halafu unakuta ziko na the sama weight. It is only fair that when you are presenting you present the people not trucks of land. That is on top of the other provision that are there in the Constitution.

Halafu kwenye hapo hapo pia kwa maneno ya uchaguzi kuna nchi kama Australia ama Israel ambazo kila mwananchi amefika miaka kumi na nane alazimishwe kupiga kura. Iwe ni lazima upige kura kama umefika miaka kumi na nane ukatae huyu ama upende ule sababu kuna wengine wanasame wanachukia maneno ya wale wanasiasa wanasema. Lakini ukimfuata huyu mtu hata apige kura that person has no right to criticize anybody he never voted for or against.

Ukiwa unapenda mimi kwenye kura enda ukubali useme unapanda huyu ukiwa unakataa tumia kura ndiyo tunasema hiyo itumiwe pia kwenye Katiba tulindwe wananchi wote waweze kuhusika katika maneno ya Serikali.

Jambo lingine ni kwamba kuwe na elaborate clause kwenye Katiba kulinda mali ya umma kutokana na watu binafusi. Wengi wanakumbuka wakati bunge ilikata ile bill ya anti-corruption ilikuwa na ile kitu inaitwa armlessly unasema tumewasamehe wale wameiba lakini hata ukisoma bibilia yenyewe inasema ukiwa umechukuwa mali ya wenyewe kwanza kabila ya kutubu na kusema umesamehewa unaenda unafanya nini? Unarudisha. Sasa hiyo haiko kwenye Katiba yetu. Ukisoma gazeti ya leo-Nation- Headline ni yule mtu ambaye alirudi America baada ya kufanya maneno ya corruption hapa wa World Bank huku yeye yuko amenzia utaratibu wa kurudisha kile aliiba kutoka mambo ile corruption aliipata hapa. Lakini swali la kwanza ni kwamba wale wa Kenya walihusika je wako wapi? Usinijibu jilize mwenyewe ndiyo tunasema iwe elaborate clause kulinda mali ya umma kutokana na wajambazi ambao wanachukuwa mamlaka.

I have a major point I was interested in – Mr. Commissioners. Na hii maneno ya Provincial Administration: Hii ilikuwa njama ya wakoloni kuwanyanyasa na kuwatawala watu weusi. Ukienda Uingereza kwenyewe hakuna Provincial Commissioners, hakuna DO, hakuna DC hakuna ma-Chief. Ukienda America na ni Katiba yetu imetoka huko kwenye (inaudible) Britain na America hakuna hayo maneno, ndiyo tungesama Bwana Commissioners Katiba yetu iweze kutambua the local authorities wawe na uwezo wa Executive powers mahali wamechaguliwa.

Mayors ama Chairman wa county council anakuwa na uwezo wa commanding authorities to the local police officer and the local police station, halafu anaweza kuendesha maneno bila hawo majambazi kutoka nje ambao wanakuja kusema hapo. Unakuta DC kuna mwizi mmoja hapa alienda kwa msitu wa Nyambene anachukuwa mbao huko anaweka nyumbani kwake. Beams zile kubwa karibu million tano ziko kwa nyumba saa hii, nyumbani. Sijui ni nani ukitaka kuuliza kidogo utajua ni nani. Ndiyo tunasema huyu mtu kama angekuwa hapa angejua atakufa hapa hawezi kufanya maneno kama hayo.

Ndiyo pia ningeweza kuunga mkono Bwana Commissioners hii hoja ya maneno ya elimu. Ukiangalia chapter five, that is the protection of fundamental rights and freedom and (inaudible) of the individual. Hiyo iko na list ya maneno mengi watu wanasema MwanaKenya ana haki zake. Hiyo pia tuongeze maneno ya elimu. Ukisoma hiyo haisemi maneno ya elimu na hata afya. Elimu na afya hizo zinafuatana.

Halafu mwisho mwisho kabisa ni maneno ya chapter six kuna hii maneno ya Kenya citizenship. Section ya 91 inasema a woman who has been married to a citizen of Kenya shall be entitled upon making application, in such manner as maybe by or under an act of Parliament, be registered as a citizen of Kenya.

Mnasikia hapo inasema a woman. There are a lot of men who have come here and married Kenyan women and they have settled here, they have invested and they would wish to be Kenyans. So hiyo pia iwe amended to recognize both mwanaume

na mwanamke.

Halafu mwisho kabisa Bwana Commissioner ningependa kusema pia maneno ya mashamba ama ya ardhi.

That land tenure system ya Kenya has been deliberately left without any policy because the weilders of powers have always wanted to steal it. Kwa Kiswahili ama kwa Kimeru

Nthii na ithaka biria twatigirwe ni bajuju na nthii iria twagwatirwe ni bakiujuju ibwiritwe kumenyerwa. Nyambene county council mwaka muthiru mwaka juria jungi bageta bakauga bakugita yonthe na bakunenkerwa nyomoo. Na bari na power nibukumenya bwibwingwa kiri shiria ya local authority county council iri na power cia kugita kithaka na ikanenkanira nicio tukuga nandi niunto turi na kaanya gakwaria. Nyomoo ii ni ciakua nyomoo rimwe, nichunanwe na power iu trust land ithirwe ni public trustee iritwe kiinya kiri county council, public trustee therwe niwe uri incharge of all that land na kwithirwe kwina difined powers cia nuu ubwiritwe kuejana, niuntu mwanka thaa ii the boss agiua nakwenda gukua acre ngiri fifety agakunenkerwa atikuria kethirwa ni ruuji ruri kuo kana ni makuyu jarikuo kana ni ingangi birikuo kana kurina anything for prosperity irikuo.

Na ya mwisho buru ni mantu ja environment, bwana commissioners masingira yetu ni jabwiritwe gukarua ndene ya katiba ujauria tugukaria maisha ja antu, niuntu tukeja kuthukia environment, our future generation itithirwa iri na kaanya kana chance ya gutura mono mono baria baari mwithu jwa Ngaya kana na mwithu jwa Nyambene bwiji bwithe jukeja kuthira guti kinya miraa buanda guku itikura kairi, guti mbura bwona ringi, bwithirwa bukari ja Mandela kana Wajir. Kwaou nitukwenda katiba itukarie kiri mantu ja masingira kiinya jo, kwaou bwana commissioner ntigukari na jamaingi kiinya kethirwa tukethirwa turi na chance ya kwaria collumune iingi inkwenda bwi bwona kaanya gakuejana maoni jenu na butikaigua buri bwingwa na teka iri rasima mbithirwe ndio nika nkwenenda tu kwonania ndiamwe na babwi na moini jaria bukuejana ni sawasawa. Asante.

Com. Ratanya: --- mafupi na marefu kidogo lakini asante yametusaia. Umesema marefu lakini ni mazuri. Mheshimiwa, I think you need to go there Mheshimiwa and sign the register. Okay, baada ya Mheshimiwa amesema mengi lakini mengi yanatuzaidia zote. Kwa hivyo tutaenda kwa mwingine hapa anaitwa Pual Kidhia. Paul Kidhia.

Paul Kidhia: Kwa majina naitwa Paul Kidhia. Nataja kuongea juu ya Majimbo: Serikali ya Majimbo isiwekwe katika Katiba yetu kwa maana kuna ukoo mwingine ni maskini ambao ukitengwa utaendelea kuumia. Na ule mchango mwingine inaendelea kuchangia ni kusema katika kuweka Katiba, Serikali ya wilaya ile kodi inalipishwa katika mahali pale, iwe ikiendelea kutengeneza mahali pale. Kwa upande wa kodi za Serikali nazo, Serikali isilipishe kodi zaidi, ilipishe kodi kulingana na vile-na kusaidia wananchi waliolipa kodi. Sina mengine.

Com. Ratanya: Okay sasa tunaenda kwa huyo anaitwa Joel Ipiano.

Joel Ipiano: Asante sana WanaCommissioners. Kwa majina Joel Ipiano. On Constitutional Review, kwanza ni mambo ya

Presidential established Commissions to investigate on issues like the Ouko murder, tribal clashes, mambo ya cattle rustling, those Commissions, have spent lot of money, that has run the economy of this country down. So those reports should be made public, and once made public, action should be taken or if not, none should be established.

Environment: We have had a lot of soil and water wastage, that there is no soil and water conservation. I don't know whether the Minister for agriculture has forgotten his duties. But let me ask through this Commission. We had hills like those which were looking like forests in the past, but these days they have been dug, no planting of trees, no digging of terraces, so this has caused a lot of havoc to many farmers, where there is eroding of soil, (Inaudible) of people's farms leaving them with nothing. So this one must be taken seriously, that the Government should ensure that there is complete control of soil and water erosion.

In a way they can compensate those people who have been allocated those places and then the government take care of them.

Cattle rustling: this one has caused a lot of insecurity. I am proposing that where there is stealing of cattle the owners of the cattle be compensated and if the owners happen to be killed in cause the government should compensate because there is no security offered as concerned to the rearing of cattle in these places or in all over of the country.

I am also proposing that there should be age limit of retirement to the Members of Parliament. You see one is ageing and becomes 60, 70 he becomes like a small child so there should be age limit that you retire at the age of 60. Also the terms of office for the Members of Parliament must have a limit 2 terms, there are other leaders who are capable also leading the public.

Education: I would like the quota system to be abolished. There is also free education: freedom education to many Kenyans means nothing, because you find that a parent has everything to do for their child to get education in our Primary schools. So when you talk of free education it must be free education in total, where the government supplies text books like in the past years. This one happened some years back. Maybe the parents can be left to provide uniform and maybe--, Okay thank you.

The other one is on those who will complete schools let us say form four, university e.t.c. I think we have a lot of people which also becomes and discouragement. Parents get discouraged when they find their children tamacking now and then. The government should at least find a way of paying those people something to keep them if they have satisfied what is required. You also find in our country that there are aged people men and women who have no relatives, no sons there should be an establishment of a home where those people can be taken care of. Thank you very much.

Com. Ratanya: Asante sana Bwana Joel. Tutaenda kwa mwingine anaitwa Pascal Mberu, Pascal Mberu yuko? Okay George Kariuki, huyo ni observer lakini kuna Makuyu Meme yuko? Then we have Hon. Joseph Mutulia. Joseph Mutulia.

Joseph Mutulia: Wana Commissioners na team yako yote pamoja na wananchi wote wale wamekuja hapa Ntonyiri yangu yatakuwa mafupi.

Kwa jina ni Joseph Muturia mwenye kiti wa National Water (inaudible) Board na Secretary wa KANU katika Nyambere Meru North. Thank you very much Bwana Commissioner kwa kunipatia nafasi hii na mimi nitoe yangu maoni kidogo najua mengi yamezungumzwa na huenda tukarudia mengine na ukisikia ati tumerudia mengine ni kusema kwamba yule alisema mbele alikuwa na maoni kama hayo na itakuwa na maoni ya mhimu.

Yangu nitaanzia na kitu kinaitwa Miraa.

Com. Ratanya: ----- (inaudible)

Hon. Joseph: Yes sir

Com. Ratanya: Kabila ya kuendela na kutoa maoni yako tulikuwa tumesema hapo mbeleni tumesam asubuhi tumpa kila mtu dakika tano, kwa hivyo limit your -----

Hon. Joseph: Mimi ninajua kuna wengine walichukuwa dakika tatu, mbili kwa hiyo hiyo pengine nitachukuwa ----

Com. Ratanya: Dakika kumi? Okay

Hon. Joseph: Asante sana, Thank you very much.

Sasa kwa ufupi nitanzia ni kitu kinaitwa Miraa Bwana Commissioner.

Miraa ni mtu ambao umeishi kwa miaka mingi katika dunia ya Africa na katika dunia ya China na hata katika dunia Middel East. Kwa hivyo nikisema vile ninasema mira nchi ile number one kwa Miraa katika ulimwengu ni China (People's Republic of China). Ikifuatwa na Republic of Euthiopia, kutoka hapo ni Kenya, halafu kutoka hapo ni Yemen hii nyingine ni kidogo kidogo mpaka South America. Sasa huyu mtu anaitwa Mkoloni amepigana na Miraa kutoka mwaka wa 1887. Professors wa Dunia wamejaribu kuharibu Miraa ma- Professors 21 katikati mwaka wa 1887 na 1983, na kile wanatafuta ni kitu kama bangi. Wanatafuta kitu kama bangi lakini hiyo wote wameshindwa. kila mmoja anapata PHD akitafuta bangi, lakini akishindwa anaweka jina lake, anaenda.

Kwa hivyo ndio tukaja mpaka mwaka wa 1948, 1946 wakati Mkoloni alikuwa na estate ya Kahawa Ruiru, Thika na Nyeri. Alipanda Kahawa alikuwa hana factory ya ku-process Kahawa, kwa hivyo alikuwa anauza mbuni na soko lake kubwa lilikuwa Middle East. Alikuwa ameona siku hizo hakukuwa na mambo ya pesa ya kufanya transaction ya pesa aki – bank. Kwa hivyo alikuwa anabeba pesa mwarabu alikuwa na pesa zake na gunia anakuja nazo mpaka Mombasa, Mzungu naye settler wa Kahawa anabeba yake mpaka Mombasa wanakutana. Anachukuwa pesa, Mwarabu anachukuwa miraa.

Na siku hizo Kahawa ilikuwa muhimu sana, hakukuwa na mwa-Africa ambaye alikuwa na ruhusa ya kupanda Kahawa.

Lazima ufanye application juzi juzi walikubali tu Kisii na Meru. Sasa wakati Mzungu Kahawa yake inaenda Mwarabu naye akaona Miraa. Sasa walikuwa wanachukuwa miraa Yemeni na walikuwa wanachukuwa Miraa Ethiopia. Na hiyo Miraa ya Ethiopia na Yemeni hakukuwa na utamu kama hii ya Kenya. Kwa hivyo Mwarabu akabadilisha kidogo badala ya kuchukuwa Kahawa, akapunguza kiasi cha Kahawa, akaanza kuchukua Miraa.

Basi kutoka hapo ikaendelea kukuwa kidogo mpaka Mwarabu akaingia miraa full time. Mzungu alipoona hivyo 1946, alitafuta njia ya kuharibu miraa akashindwa. Basi alikuja hapa NFD Isiolo mahali kuliwa na PC wa NFD, aka-organizewanawake wa Somali na wa Borana, akawambia wapeleke delegation kwa governor na msememe maneno haya nimi nasema. Msememe mabwana zenu wamekataa kurudi nyumbani wanakula Miraa mpaka usiku kucha, na ile kazi inatakiwa na ni national duty, ile kazi ya kitaifa ya kutengeneza watoto, hao wanaume wamekataa. (Clapping) sasa-na hiyo iko katika record za archives ya Kenya. Basi Mzungu sasa kusikia hayo maneno, basi akapata nguvu ya kuweka hayo mambo ya Miraa katika legico, ili kwamba wapige marufuku Miraa, wakisingizia kwamba hii Miraa inajaribu kuharibu wanaume wasiende ku— (Laughter) sasa hiyo imechukuliwa.

Com. Ratanya: Toa mapendekezo Bwana— pendekezo kabisa kabisa

Hon. Joseph: Sasa pendekezo hili ni kwamba katika Katiba yetu ya Kenya kila mtu katika nchi ana Miti yake na hata hii miti tunapata dawa zote ambacho hakuna ugonjwa isipokuwa ukimwi haujapata dawa hii miti ingine yote ina---- ugonjwa ingine yote iko na dawa na kwa hivyo kuna ile miti ile protective ile inasemwa huu mti hata usikatekate ovyo ovyo kwa sababu una dawa na Miraa ina dawa ilikuwa ina ina a great asthma hakuna mtu wa hapa ako na asima. Miraa inaondoa ile common cold.

Com. Ratanya: Sasa unapendekeza nini Mheshimiwa?

Hon. Joseph: Napendekeza Miraa ichungwe kwa (inaudible) iwe protected kabisa. Isije ikawa na kitu kingine, iwekwe ndani ya Katiba katikati ili kwamba hakuna mtu ambaye kuifanya hata kidogo.

Basi ya pili Bwana Commissioner ni mipaka ya Meru. In 1963 ilipoingia ndiyo sasa Katiba ya sasa iliarabu mipaka ya Meru. Shida ilikuwa ni kwamba mpaka wa Meru mpaka wake ulikuwa Kariobatula. Mpaka wa Meru ulikuwa Isiolo ilikuwa ndani ya meru. Na hata saa hii ukiangalia Isiolo county council ilikiwa inakodeshwa na Meru county council shilling eight thousand shillings kwa mwaka kulisha mpaka Isiolo na sasa hiyo mpaka hata isiolo ndani ukiangalia map ya Meru utaona vile kamekuwa kama matiti ya ng'ombe kameingizwa ile iwe headquarter ya Isiolo. Wana Commissioners tunasema mpaka wa Meru urudi mahali ilikuwa zamani hiyo ndiyo recommendation yangu.

Ya tatu, kuna kitu kinaitwa Presidential election. Wakati Rais ametangaza mimi nitafanya- kwa sababu kuna Parties ziko hapa Kenya zetu, kuna Parties kama KANU, kuna DP, kuna NDP (Ilikuwa KANU hiyo), kuna FORD KENYA, kuna hizo zingine. Sasa, yule ambaye atataka kuwa President, iandikwe katika Katiba Bwana Commissioner kwamba, President akitaka

kusimama election, na yeye ataje Vice President (Clapping),yule ambaye watakwenda na yeye, akishindwa washindwe pamoja.Akishinda washinde pamoja ili taifa liwe linajua ni nani atakuwa Vice President, awe anachunguzwa kuanzia mwanzo.Kwa hivyo kama KANU inataka kuchukuwa President, yule wa KANU achague Vice- President wake, yule wa DP achague , yule wa FORD KENYA achague wake, basi waende namna hiyo.So that wakati uchaguzi unakwisha, basi tumepata President na Vice-President automatic.

Com. Ratanya: Baado dakika tatu Mheshimiwa.

Hon. Joseph: Asante sana. Sasa ile ingine katika Kenya---

Com. Ratanya: Kwa hivyo maaliza hiyo kwa dakika kama mbili hivi.

Hon. Joseph: Hiyo ingine ni ,katika Katiba ya Kenya, I recommend kuwe na Prime Minister na huyo Prime Minister asiwe appointed na mtu yeyote awe ni Bunge linafanya appointment ya Prime Minister ili aki-mess kama analeta wasi wasi au mambo ingine Bunge linapiga kura linatoa imani yao kwake ili serikali ingine President ambiwe sasa hiyo imekwisha leta ingine.

Com. Ratanya: Ya mwisho –

Hon. Joseph: ya mwisho Bwana Commissioner ni mambo ya Katiba.Katiba ya 1963 ilimalizika kwa mwezi moja na ilikuwa mbali sana London Lancaster House tunaomba kwamba hii Kitabu tafadhali Bwana Commissioner mjikaze sana mkasee sokisi mkasee kila kitu hii Katiba imalizikia before December kuwe na elections.Ya mwisho kabisa, do you get me that -----(interjection) mwisho kabisa.

Hon. Joseph: Mwisho kabisa kabisa. Katika Kenya kuna post ya PC, kuna DC, kuna DO, kuna Chief kuna Assistant Chief, na hao watu ile kazi wanafanya si wao wanafanya. Kuna watu wanaitwa Sub-areas. Bwana Commissioner, hawa ma-Sub-areas pia wawe katika Katiba, wawe recognized by our Constitution, yaani watambulike kwamba wako na Serikali si Chiefs peke yake.Kwa sababu Chief akichukia huyu anamtoa.Wawe recognized na wajulishwe kabisa ni watu wa utawala, kwa sababu wanasadia ma- Chief na Assistant Chiefs mambo ya utawala.Kwa hivyo na pia wawe wanapata kitu kidogo inform of allowances, kama vile committee za land kama vile committee za county council, wanapata hicho kitu. Sasa nikimaliza ninasema ninakushukuru pamoja na mwenzako kwa kunipatia hii nafasi ingawa umenikimbiza sana. Thank you.

Com. Ratanya: Makuyu Meme Yuko? Makuyu. Makuyu Meme--- ni wewe Makuyu Meme.

Makuyu Meme: Riitwa mbitagwa Makuyu Meme.

Translator: My name is Makuyu Meme.

Makuyu Meme: Ndiuga atiri, ekuru ni tuinyiragua mono batwii.

Translator: I am saying that we women we have been oppressed for a very long time.

Makuyu Meme: Niuntu bwa akuru betu beeta naja obicine bakendagia ithaka tugatigwa utheri tugatigwa na thiina na twana.

Translator: Because during the issue of title deeds it is only the name of the husband that appears, and then the husband may sell the land without assent from the wife. So we are suggesting that during the issue of title deeds, two names must appear so that one of the people should not just share the land the way you want.

Makuyu Meme: Na ringi biria turatetagira mono, twatetagira oo ithaka biu bikujukua bikendua tugatigwa thinene ekuru bagatigwa thinene na twana tugatigwa thinene.

Translator: So since this has been the problem, we are suggesting that let us have a provision or in the Constitution that you are making, let that Constitution protect us from this problem.

Makuyu Meme: Biria bia tumaga twinga mukoroni twamwingaga niuntu bwa ithaka biu kenda turijaga uhuru batwi.

Translator: This was the main reason that was making us fight for the freedom of this country- to get our land and live in it peacefully.

Makuyu Meme: Nibwo jontu uuni ngutetaa na ringi tuckerwa batwi ikundi bia ekuru batwi kuririo tuthethagua kuririi turatethagua baria barujagira ukoroni beejwaga kiinya ithaka na bagatethua baria bati na iinya riu rii tutitethagua.

Translator: We are also saying that we the women groups should be assisted as it used to be before. In the past the Government used to assist us through the women groups. So we are suggesting, let us have a provision or let us have somewhere in the Constitution, that we will be protected and have a way to help us.

Makuyu Meme: Na bii tugutetura batwi tutiumba kurega gutetera miraa, miraa niyo tuendete kiinya Kenyatta itwamwira oriu nitwamwonagia iinto biria biumba guthethia Kenya.

Translator: The land point is about the Miraa. We are also advocating that there must be a provision to protect Miraa, because even during the last regime we were advocating for the same thing, because Miraa has actually helped this place. Thank you so much.

Com. Ratanya: Tunaweza kwenda kwa mwingine hapa anaitwa Isaiah Kibuli, naona kama hayuko, ama yuko karibu. Bornface Mbavu, George Karuti, John Itiame. Yako ni jina gani? George Karuti.

George Karuti: Jina langu ni George Karuti. Yangu ni haya. Nilitumwa na hawo vijana wa rika la (Inaudible) wakaniambia kuwa niwauliziekama kuna nafasi wanawezapata kwa serikali, wakati wanaweza ungana vikundi vikundi, na kuungana kiasi ambacho wanaweza kupata mtu wa kuwafikisha kwa serikali, wapewe loan ndiyo wawe wanafanya kazi.

Lengine ni hili. Kwa hawa vijana kama vile Mr. Muregi alisema ati katika hii county council ya Nyambene watakuwa wakichagua vijana wale watakuwa home guards hawo vijana ikiwezekana serikali yetu iwahusishe kwa hiyo kazi ni hayo tu sina mengine.

Com. Ratanya: Tumesikia mambo. Joel Muchane? Dennis Muthee? Charles Kiringi? Charles Kiriangi. Gideon Kobia Gideon.

Gideon Kobia: Mimi naitwa Gideon Kobia ningetaka kutoa hii maoni ili ingizwe katika Katiba inatarajiwa kuundwa.

Kwanza ni elimu: Vitabu vya shule visibadilishwe kila mwaka kama vile inavyoendelea wakati huu. Kila kitabu kikiwekwa katika utaritabu wa masomo kitumike kwa miaka mitano ama miaka nane. Walimu wawe wakiajiriwa kila mwaka. Watoto werevu wapewe misaada kutoka kwa serikali na mashirika mengine.

Vita vya ukabila vikomeshwe na serikali. Mipaka ilindwe ya kabila lolote. Hatutaki wakimbizi katika hii nchi yetu. Wakimbizi hawa wanaletwa na vita vya makabila mengine. Mwananchi wa Kenya ana haki ya kukaa pahali popote katika nchi yetu.

Hapa Kenya hatutaki serikali ya Majimbo, kwa sababu nchi yetu ya Kenya iko na makabila mengi.

Wakuu wa Mikoa wateuliwe kwa masomo waliofuzu kutoka chuo kikuu. Wakuu hao wawe wakitembelea hata sehemu ndogo kama sasa.

Com. Ratanya: Kama ni juu ya vitabu pengine ungefanya summaryongee machache. Dakika moja imebaki.

Gideon : Haya. Rais awe akitumika kwa miaka 55 hapana zaidi. Si vizuri mtu kuwa Raisi au achaguliwe kuwa Raisi akiwa ajasoma hata chuo kikuu.

Na waziri wachakuliwe kulingana na masoma waliopata.

Uchaguzi uwe uhuru na haki. Sina mengine.

Com. Ratanya: Asante sana Gideon. Andah Mwet, Andah Mwet yuko. Mwingine ni Joseph Mithika ? Joseph Mithika endelea.

. (interjection) utakaa ama utasimama)

Joseph Mithika: Wacha nikae tu. Jina langu ni Joseph Mithika:

Maneno yangu ya kwanza ni hii watu wa Chief. Pahali pa Chief na sub-Chief uondolewe ama akizidi akae wawe wakienda transfer kama wafanye kazi wengine wa serikali siyo Chief amalize miaka 55 kwa office peke yake.

Mbunge: Mtu akishindwa kuwa na kura asichaguliwe Mbunge maalumu.

Mtu aki-retire asipewe kazi ingine ya serikali kwa sababu kuna vijana wengi hawana kazi. Asanteni sina munge.

Com. Ratanya: Okay, asante sana. Tunataka namna hiyo kwa ufupi na mambo yako ya kweli. Kwa hivyo tuende kwa mwingine huyu anaitwa Isaiah Kaenga. Isaiah Kaenga yuko. Kama Isaiah hayuko tuna Gitonga Stanly. Gitonga Stanly hayuko. Kuna Cypriano Maore? Cyprian Maore? Ni wewe Cypriano? Gitonga Stanley. Endelea.

Gitonga Stanley: My views are that the government should outlaw genital mutilations for girls who are under 16 years.

The government also should root out corruption in all sectors by vanishing those court taking--- or giving price serverely.

(interjection) Ongea Kwa sauti.

Gitonga Stanley: All children should have equal Right to inherit land irrespective of their agender.

Majimboism should not be allowed in this country.

The government should tighten security in all parts of the country so that cattle rustlers are brought to book wherever they commit the crime. The powers of the President should be reduced. Many Thanks.

Com. Ratanya: Okay, asante sana Gitonga. Cyprian Mwaore?

Cyprian Maore: Kwa jina ni Cyprian Maore.

(interjection) Unataka kukaa

Cyprian Maore: Yes. Ningetoa pendekezo yangu kuhusu kwa upande wa Judicial ama wa Sheria.

Ningetaka Rais asikuwe na uwezo wa kuchagua Judge Mkuu, iwe ni idara ya Mahakimu ya kuchagua Judge Mkuu, ndiyo ikuwe na justice.

Ningetoa proposal nyengine kuhusu sheria ile, ikiwe mtu wa Serikali amekosea ni lazima uende kwa Attorney General ndiyo upewe barua ya kumushitaki. Ningependelea ikuwe huru, mtu yeyote akashitakiwe ikiwa amekosea. Sina mengi ni hayo tu.

Com. Ratanya: Tunashukuru sana kwa hayo mengi na ni mazuri haya umetaja. Sasa tuende kwa Isaiah idani ? Isaiah Idani yuko? Hayuko. Hosea Akubia, Hosea hayuko. Joel Mbavu, Joel Mbavu, Joel hayuko. Francis Mjumbe? Na huyu nyumae ni obsever Kaveria na Peter ni oberver lakini kuna Charles moria, Charles Moria . Are you Chales Moria?

Charles moria: Mimi ninaitwa Charles Moria na ninataka kuto maoni yatengenezwe katika Katiba Mpya. Kama vile imesemwa ya Miraa, Miraa iwe secured katika Katiba ya nchi yetu.

Security , mwananchi pamoja na mali yake awe secured.

Political Parties: ziwe mbili, siziwe nyingi sana kwa sababu zinawachanganya watu.

Presidential power: Rais awe chini ya sheria, chini ya Katiba kama vile tunaona hata kanisani hata pope ako chini ya

Constitution ya kanisa hata President asiwe overpower over the law.

Hatutaki serikali ya Majimbo.

Executive, Judiciary na Legislature ziwe uhuru. Executive isingilie hao wengine.

Education: The government should provide free education. Kama vitabu, na health, na land. Land ni common good na hatutaki mtu mmoja awe na ekari elfu moja na kuna mwingine hapa ako hata na point 50.

Sasa kwa land wale wako na ekari kubwa sana zigawanywe kwa wale hawana.

Corruption: Kuna ufidadi mwingi sana katika serikali yetu ya Kenya-kama mtu anataka kuajiriwa kama mwalimu ama kwa police, anatoa elfu 30 ama 50 thousand, ama hata mtu akitaka university college anatoa pesa. Ufidadi usiwe katika nchi yetu.

Ingingine ni haki ya kuishi: Kila mwananchi ako na haki ya kuishi. Hatutaki abortion iwe legalized as it is said in the NGOs.

Com. Ratanya: Kwa hivyo jaribu kumaliza.

Charles Moria: Nimemaliza sina mengine.

Com. Ratanya : Sasa tuna Stanley Njuki: Na useme jina lako Stanley.

Stanley Njoki Mugambi: Kwa majina naitwa Stanley Njoki Mugambi. Mimi nikiwa mwana Kenya halisi maoni yangu kuhusu Katiba ningetaka kusema hii. Sisi tulindwe kama wakenya wengine. Ng'ombe zetu zimeingiliwa na wezi kila siku sisi hatulali usiku na mchana mahali tunapata kwa kuchunga Ng'ombe lakini wezi wanatuangaisha sana.

Miraa yetu sisi tukiwa watu wa Nyambene huo mmea ni mzuri, ni kama Majani Chai na Kahawa pia Miraa ikiwa mbaya hata Majani na Kahawa iambiwe ni mbaya. Sina mengine hayo ndiyo maoni yangu.

Com. Ratanya: Okay, asante sana Stanley Njoki. Sasa kuna Daniel Inyinge is a Retired Officer. Sasa Daniel wakati ni wako sasa, lakini dakika tano tu mzee. Okay, endelea, endelea Daniel. (interjection) Utasimama ama utakaa.

Daniel Inyinge: Nitasimama.

Daniel Inyinge: Okay asante sana Bwana Commissioner. Kwa majina naitwa Daniel Inyinge na tena naitwa Kibanga. Mahali unaona tuko sasa hivi hapa ni Laari katika Ntonyiri Constituency. Lakini kile tunachangia ni Katiba ya Kenya marekebisho ya Katiba ya Kenya. Kwa hivyo Bwana Commissioner ningetaka kuchangia hii maneno ya Katiba ya Kenya kuhusu economy, economy ya nchi hii imeharibika na Katiba isipochunga uchumi wa nchi hakuna nchi hakuna Katiba. Kwa hivyo kama munataka kuchunga economy ya nchi, lazima kuwe na few Ministries, the Ministries are so many in Kenya that they are using a lot of money within those Ministries n watoto wetu hawandikwi kazi kwa sababu unaona kila Ministry iko na Assistance

Ministers, Ministry iko na magari mengi na ile kazi anafanya hakuna kwa hivyo Bwana Commissioner lazima Katiba ya Kenya ichunge economy ya nchi na economy----

Com. Ratanya: Umependekeza wawe wa ngapi, Minister wawil au kumi au wangapi?

Daniel Inyinge: Ministers wawe kama watano hivi katika hii nchi ili pesa zipatikane na Ministry iwe na Assitane Minister mmoja na awe na magari y kutumia siyo meng ya kumaliza pesa.

Kwa hivyo Bwana Commissioner hii economy ikiwa sawa watoto wetu wale wamemaliza college, wengine wamemaliza kidato cha nne wakamaliza college lakini wanalala nyumbani kwa sababu economy ni poor kila mtu akienda hapa economy ni poor haiwezi nzuri kama kuna pesa ya kutumia bure.

Powers of the President: The President is so powerful that anaweza kukuteremusha madaraka mara moja, anaweza kukupandisha madaraka moja, kwa hivyo kama mtu anapandisha mara moja ni mzuri lakini akiteremusha mara moja si atakufa? Kwa hivyo iwe ni Katiba ina President ambaye apandishi watu mara moja na awateremushi mara moja.

Com. Ratanya: Pendekeza

Daniel Inyinge: President awe hakuna kuteremsha mtu madaraka mara moja. Awe anachunguzwa aone kama atapandishwa cheo ama kama atateremushwa cheo, siyo mara moja.

Mambo ya kuchunga Katiba lazima yawe implemented. Tukitengeneza hii Katiba iwe implemented kwa sababu ile Katiba ilikuwa imeandikwa ilikuwa inasema itachunga afya ya mwananchi haijachungwa. Ilikuwa imesema itachunga security ya mwananchi, security haijachungwa. Ilikuwa inasema itachungwa education ya wanananchi wote haijachungwa kwa hivyo ile Katiba tutatengeneza sasa iwe ni Katiba ya kutumika siyo ya kuandikwa.

Kitu ingine kile ningesema ni kuhusu wazee. Kuna wazee ambao wameanda retire kama mimi wengine wametoka katika Ministry mbali mbali na lazima wapatiwe heshima na economy ikiwa mzuri hata hao retire wawe wakiongezewa kitu kitu kidogo mukiwa mumesha andika watoto wale wamemaliza shule kama economy ni mzuri halafu mrudi muangalie wazee na hata wazee wale bado kuandikwa bado ku-retire kama wale wenye miraa hii wawe wanachungwa kwa sababu nchi ingine katika dunia hii zinachunga wazee Katiba yao inachunga wazee na kwa hivyo Bwana Commissioner ningependekeza Katiba yetu ya Kenya iwe inachunga wazee, wazee wale wamepanda hii Miraa, wachungwe na njia ya kuchunga Miraa yao hamtakuja kuwaongezea mshahara kwa sababu hawajandikwa lakini mkichunga Miraa yao mtakua mumechungu wazee wa Miraa ile Katiba ya zamani cap. 339 ile ilikuwa ya mkoloni iliondolewa na Haiyati Mzee Jomo Kenyatta mwaka wa 1977 January 17th ilikuwa ni January 17 ndiyo hiyo cap 399 ya mkoloni iliondolewa na huyo mzee Jomo Kenyatta katika State House Nakuru wakati alitembelewa na wazee wenye Miraa na Mzee huyo Haiyati Kenyatta alipatiwa Miraa n Bwana Muturia na akatafuna

hiyo Miraa na hakuaribika na ni President kwa hivyo kama hiyo cap ilipotea ipotea kabisa kabisa katika Katiba hii na mtakuwa sasa ikipotea mtakuwa mumechunga wazee wenye mashamba ya Miraa. Asante sana Bwana Commissioner. Kwa jina naitwa Daniel Ntonyinge Kibanga.

Com. Ratanya: Asante sana Bwana Kibanga kwa hayo maoni yako kwa hivyo sasa tutaenda kwa Richard Mbabu, kama Richard hauko tuendelea kwa mwingine, kuna Kabwe Syllas, Kabwe Syllus huyo ni observer. Richard Mbabu ameingia.

(interjection) Unaitwa Richard? Sema jina

Richard Mbabu: Jina langu mimi naitwa Richard Mbabu. Maoni yangu ni haya. Mimi vile napendekeza hii nchi yetu ambayo tuko nayo tulipigania ili tupate haki. Ningependelea kila mmoja awe na haki ya kwamba yeye yuko na haki katika nchi yake. Unajua ukisikia kama wewe una haki ya nchi yako utaona vibaya yaani kwamba una haki. Kama mwananchi anatembea barabarani asiwe akikutana na askari anamchapa mbao bila kuwa na makosa.

Ya pili kuna pombe yetu inaitwa marua ambaye si pombe ya haramu, ningesema hiyo Marua tuwe tukubaliwa tunakunyua maana yake---. Nimemaliza maoini yangu.

Com. Ratanya: Okay sasa, wananchi hebu nyamezeni halafu tuendelea. Kuna Simoni Meme, Simon Meme yuko, can you see whether he is coming. Samson Ntomungania?

(interjection) Useme jina

Samson Ntomungania: Mbitagwa Charles Mungania, naninkwenda muntu uria ukaria na giswahili ntimenya giswahili nkaaria na kimeru.

Translator: I am Charles Mungania.

Samson Mungania: Na ndienda kuuga uria kuuga bwa gatiba ya Kenya ndienda kuuga muntu igwitwa DC naewe jukumu inene niuntu niwe uriragirwa ni antu baria baranjirua kuthukua kuu ni committee baendu kiinya kiri machief na kiri bangi bonthe bakaingiliwa ni DC niwe ubatethagia ja uuni ni ntethagua ni DC.

Translator: What I am proposing to the Constitution that we are making that we are in the process of making is that the office of the DC should be an office of responsibility let that person who will be elected --- let us have a law that says that whoever is to own that office must be someone of responsibility because this is an office that us in grass root connection to the people.

Samson Mungania: Uuni ndikurikia gutethua ni DC ampa baruga ndeeta mwanka kwa njuri, ndigwita kwa njuri muunda jwatui jwakwa ndacoka antu baeta baukumana kairi ndacoka ndaumara oo ndeeja muunda ndarega nkunenkerwa. Kireii, nika

bukaigua muntu utiji kwaria neka butikiira akaria, nijo nkwaria haya kuuma au muunda jukurema ndikuuma au na ndikunenkerwa ndaita mwanka human right haki ya binandamu.

Translator: You find the reason I am emphasizing that the office of the District Commissioner should be an office that is possibility of that type is the reason is that its an office that have actually helped me and I have a testimony of what it means to be in that office so I am emphasizing that office to be an office that should be protected in the new Constitution.

Samson Mungania: Ndikurikia gwita ndeerwa muntu uu human right haki ya binandamu atukuu na atija kuu ugwe nyomba yaku gatukugitana na (inaudible)..... Ndachoka ndeeta gwa commissioner ringi.

Translator: There is a time I had been oppressed for long time---

Samson Mungania: Ndiena bwa miunga kubwa niuntu ninkwona batwi tuthithagua uu muntu athimirwa muunda jwawe kethirwa nijukiringwa nthii niuntu juu nakuria jugachoka jukagitwa pupblic, public ithano kaa puplic ithatu.

Translator: My second point concerns the issue of land. We are saying that the demarcation of land has been a big problem in this area. We are saying let us have a law or a policy that actually will protect the people at the end of the day as we make this Constitution. Thank you so much.

Com. Ratanya: Okay, kuna Julius Kabira. Na mtu sasa akiitwa, ukisikia jina lako kama uko hapa ufanye mkono namna hii tujue msipige kelele kama hayuko hapo halafu tuta-council na hautarudiwa tena . Kwa Julius Kabira hayuko. Tabitha Kario yuko? Okay Tabitha kuja.

(inaudible) asubuhi tulipokuwa tumekubaliana mashariti ambayo tumekubaliana ya watu kutoa maoni yao, shariti la kwanza au mipaka ya kwanza tulioweka ni kwamba akaja mtu kutoa maoni yake hapa hata wewe ukawa hufurahii maoni hayo, au unaona maoni haya hayana maana; huna ruhusa kumwingilia huko, kumpigia kelele, halafu tunaenda hivyo kazi inakuwa rahisi. Mkinyamaza vile mnisizikize mnavyonisikiza mimi na nawashukuru kwa kunipa heshima hiyo, mkampa bibi huyu heshima namna hiyo, kazi hii tutaimaliza haraka na kila mtu atakwenda nyumbani amefurahi kwa sababu ametoa maoni yako. Au si sawa hivi? Basi twendelea.

Tabitha Ngariu Ngore: My name is Tabitha Ngariu Ngore. My proposals are.

All women should be honoured because on the side of the land men sell their land and they ask us if we came with land from our fathers. So in this Constitution I would like a provision to be enacted in the Constitution.

The elected MP: We would like the MP whom we are going to elect to have their office in their Constituency where anybody can see him . Those are my proposals. Thank you.

Com. Ratanya: Mwingine anafuata ni Edward Mwicha. Edward kama hakuna mkono ninaona huyo hayuko. John Kang'etu? John Kang'etu. Joseph Kitaitari, Joseph Kinyua, Charles Kichugu. Charles ingia ni wakati wako.

Charles Kichugu: Mimi naitwa Charles Musungu.

Ningependa kupendekeza ya kwamba Katiba ya sasa iandikwe iwe ikisomwa primary and secondary ndiyo wananchi wapate kujua (inaudible).

Ningependa kusema police wazungushwe, wana uwezo mwingi sana, wanaweza kukukamata wewe na wakushitaki wewe kwa kile kitu hata hujafanya. Hata huyo police ukimushinda kwa mahakama awe anakulipa kitu, au serikali inakulipa wewe maana yake anakuweka bure.

Tunataka uwezo wa MP, MP maana yake ni mtu alichaguliwa na mwananchi na kwa wingi wanazoea kukaa Nairobi hawaonekani hapa awe sheria ipunguzwe kukuwezekana wananchi wandamane asimamizwe kazi kabila wakati kufika.

Uwezo wa sub-Chief, Chief maana yake wanatumia power yao kwa uwezo mingi sana kama ni mwananchi akiwa na makosa awe akitumiwa huwa anaitwa anapewa heshima kwa mwananchi wa kawaida. Sasa ikiwezekana anaweza kuchaguliwa na mwananchi ndiyo atambue mwananchi ndiye nani. Sina mengine ya kusema ndiyo hiyo.

Com. Ratanya: Twenda kwa Patrick Mungera, Peter Kang'endu, Simeon Mailu? John Mututwa.

John Mutua: Thank you. Kwa majina naitwa John Muta katibu wa DP Ntonyiri. Kwa maoni yangu kwanza kabisa ningetaka sheria za Rais ziwe reduced, at least asiwe na powers za ku-appoint: Chief Justice, Judges of appeal and Attorney General. Maana yake ndiyo unakuta kama ni kortini, hakuna haki tunafuata, kwa vile hao ma-Judges saa nyingine wako na yule wanataka ku-please. It is not that they are there because they are to serve the people lakini kuna yule wanataka ku-please. So Rais asiwe na uwezo wa kuwa ana-appoint hawo Judges instead kuwe na Commission ambaye itakuwa inawa-appoint na kama ni Chief Justice ama ni Attorney anaonekana afanyi kazi yake iwe ni ile ile Commission itakuwa na uwezo wa kumtoa madaraka.

Tukiangalia kwa education system yetu kama vile ilikuwa sasa hii ya 8.4.4 system tunaona ya kwamba imekuwa as per total failure. Na hii imetokana na uwezo wa mtu mmoja tu kuangalia kulala siku moja akaona education system ibadilishwe bila hata ku-consult wale ambao ni professionals. So in future in our Constitution let it be made clear that if education system has to be changed kuwe na Commission ambayo itakuwa appointed inachunguza na inaona kama kweli kuna haja ya kubadilisha hii mwenendo ya elimu.

Tukiangalia in Kenya we have been having so many Commission of inquiries zile ambazo Rais ukiwa na jambo fulani kwa vile

ana uwezo anasimama leo anasema nime-appoint this Commission of inquiry inaenda inachunguza mambo inatumia pesa ya serikali ambayo pia ni pesa ya mwananchi halafu mwishowe ikirudisha ile reports pengine Rais akiona haifai ama akubaliana na hiyo anakalia hiyo atowi ile report kwa public ambaye ni pesa ya public alitumia.

Com. Ratanya: Unapendekeza nini

John Mutua: Napendekeza in future let the Parliament be given powers to appoint the Commission of inquiry ama ikiwa kuna uwezo kuna haja hiyo Commission iwe ni Parliament itawa-appoint na ndiyo itarudishiwa results sa hiyo matokeo ya inquiry.

Kwa vile Kenya tumekuwa nchi ya multiparty, na kila chama kina haki ya kuhapa mimi ningependelea wakati wa campaign kwa vile zile pesa zinatengwa huwa ni pesa za mwananchi tax payers money every Party and every Presidential candidates awe anapewa pesa wawe wanapewa equal siyo hati kwa vile huyu ndiyo pengine alikuwa the incubate President ana uwezo wa kuchukuwa ile pesa ni kila Presidential candidates awe anapewa pesa sawa na yule mwingine na security pia awe yule security amepewa kama ni wa DP awe anapewe security kama vile wa KANU anapewa ama wa chama kile kingine wote wawe wamesawazisha.

Education system: Our state universities unakuta zote yule ana-head hizo universities anakuwa ni Vice Chancellor lakini Chancellor anakuwa ni Rais, ambaye saa nyingine hata hana degree lakini wale ana-lead ni Professors, ati ndiyo mdogo wake. Let it be that every state university be lead by a Chancellor ambaye ni wa hiyo university, ndiyo atakuwa na uwezo wa ku--- bila kuliza uwezo kwa mtu mwingine ambayo ni Rais so Rais asiwe ati ndiye kiongozi wa kila university hapa nchini.

La mwisho ni kwa wale MPs ambaye tunachugua. Saa zingine ukiangalia kwa Katiba yetu haisemi kama vile unakuta kwa wafanyi kazi wengine Katiba inasema vile wanapaswa kufanya kazi kama wafanyi kazi wa kawaida lazima wafanye kazi kutoka asubuhi wawe kazini sa kumi na moja anaondoka. Hiyo ni sheria inaleta hiyo, lakini ukiangalia kwa wabunge wetu hakuna pay day unafanya ile inaitwa technical appearance. So ningependelea ya kwamba kuwe na sheria ambayo inasema ile siku yoyote ambayo ni siku ya Bunge kukutana, at least awe ako huko kwa nusu ya masaa yale anapaswa kuwa uko, hata ikiwa si siku mzima at least a half of the day kwa kila siku ambayo anapaswa kuwa Parliament, kwa vile tunamu- elect awe kwa Parliament kutusaidia huko.

Com. Ratanya: Jaribu kumaliza.

John Mutua: Namaliza. So iwe kila MP ni compulsory awe ana-take Parliament in all the stating ndiyo kusiwe ati hakuna chorum hakina hivi iwe ni compulsory ki-sheria. Kwa haya machache ndiyo ningetaka kuchangia asante.

Com. Ratanya: Tuende kwa Pius Miriri, Pius Miriti. Okay, Miriti endelea.

Pius Miriti: Kwa majina naitwa Pius Miriti.

Kile kitu ningesema ni kwamba kuna wakati mwingine watu wanakuwa wagonjwa na wanaenda hospital, na they are admitted na wanalipa bill ya total to something to do with five hundred thousand or even a million. Sasa ningependekeza serikali ichukuwe jukumu hilo, itenge hazina fulanikwa Ministry of health, wawewakishugulikia watu kama hao. Kwa vile mwananchi wa kawaida kupata shilling elfu mia tano ama million its very hard, sasa ningependelea hazina iwekwe.

Com. Ratanya: Unapendekeza matibabu ya bure ama vipi?

Pius Miriti: Napendekeza kuwe na matibabu ya bure kwa mtu wa bill ya more than 50 thousand. Upande wa uchaguzi: Kura ziwe zinahesabiwa pale zinapigiwa siyo ati kura ziwe zinasafirishwa kwa sababu wizi wa kura unatokea barabarani ama sehemu zingine kura ziwe zinahesabiwa mali zimepigiwa. Kwa hayo machache sina mengi.

Com. Ratanya: Bwana Pius, enda kwa register uweke sign yako. Sasa tutaenda kwa Philip Mtowadheru, naona hayuko, M'tomungania Murithi? Charles M'tomungania? Charles M'tomungania yuko? Huyu tunaita ni Charles. Samson Itari kama uko hapo inua mkono halafu uje. John Mucheke. Ni wewe Mucheke sawa sawa.

John Mucheke: Kwa majina naitwa John Mucheke. Yangu ni machache tu. Nataka Katiba yetu iangalie miraa zaidi kwa maana miraa kwa upande wetu ni kitu cha maana. Sisi hata ukileta million hatuwezi kukuuzia mwanamke, lazima utoe Miraa. Sasa Miraa isi chukuliwe kama mmea mwingine kama vile maharagwe, matunda na mahindi. Saa hii naelewa ya kwamba hata serikali iziangatie miraa kama mimea mingine.

Nataka kusema tu kitu kidogo kuhusu serikali, hongo iondolewa upande wa serikali kwa maana serikali ndiyo inaleta hata umaskini sana kwa wananchi. kwa maana ukikutana na majambazi utakatwakatwa, pale ukienda kuomba usaidizi kwa serikali lazima utoe hongo, akuitishe kitu kidogo ili aondoke aende kukusaidia. Naonelea kwamba anaajiriwa, anaandikwa, anachukuwa mshahara kila mwezi, sasa anataka nini kwa mwananchi wa kawaida. Lazima amsaidia. Hongo ziangaliwe sawa sawa kwa Katiba yetu.

Tunataka kuangalia kiti --- manyumbani: Ukiangalia uhondo ni lazima uingie na uweze kuangaisha watu karibu wote nyumbani. Serikali iangalie mambo ya uhondo saana wakati ambayo unaona mtu analala hospital anatomia elfu mia na hana kiti za kulipa ile serikali imulipie kitu kidogo kwa maana tukiangalia yule mtu zaidi anaweza kuuza hata shamba yake ako na watoto watano kumi hivi na watoto wakaachwa maskini na unajua ugonjwa ni lazima wa kila mtu.

Upande wa masomo: serikali hata isaidie watu upande wa masomo. Kwa maana tunaweza kuona watu ambao wanataka

kusomeshwa lakini hawana mapato, akashindwa na kusomesha watoto. Serikali itusaidie kidogo.

Tunataka kuangalia mambo ya pombe ya haramu. Pombe ya haramu ndiyo inaleta mambo muhimu ata umasikini unaweza kuona wazee wengi wanauza mashamba yao wakienda kukunywa pombe ya haramu na wanaacha watoto bila kitu sasa nataka Katiba ipatie wazee ---

Neno la mwisho kabisa ni Chief ama sub-Chief kwa maana anaenda kuajiriwa na serikali na aingie kupewa kazi na mwananchi. Ni lazima achaguliwe na wananchi ili ata serikali ione ya kwamba yule Chief anapendwa na wananchi na akiajiriwa kazi anaenda kutoa (inaudible) wakiwa pamoja na wananchi.

Com. Ratanya: Okay asante sana Bwana John Mucheke. Tuliacha Charles Mungania lakini tunatafuta jina lako. Huyu amemaliza ni John Mucheke lakini kuna mwingin tuliacha hapa anaitwa Joseph Kamayi yuko?

Joseph Kamanu: Bwana Commissioner, jina langu mimi naitwa Joseph Kamayi.

Com. Ratanya: Endelea Joseph.

Joseph Kamayi: Vile mimi naomba ma-Chief na ma-Sub-chief wachaguliwe kwa siri. Miraa: Miraa ndiyo kitu important ya kutusaidia kuliko vitu vingine Ntonyiri hii.

Com. Ratanya: Okay asante sana Kamayi inaonekana (inaudible).

Joseph Kamayi: Ile ninasema Miraa iwekwe maanani zaidi.

Com Ratanya: (inaudible) Joseph asante sana tumesikia hiyo ----- weka hapo uweke sign yako hapo. Wananchi kuna mambo ningetaka kuakumbusha. Tumesikia mengi yale ambayo yamesemwa na wengine na yale pengine mtasema baadaye lakini kama unasikia kwamba mengine yalisemwa kama Miraa badala ya kusema story yote ya Miraa nikusema ya kwamba unaunga Miraa uwe sawa sawa kama wale wengine na umalizie wapi hapo badala ya kusema tunatumia ya kwenda kuoia nini na yote tunajua tumeambiwa, si tumeambiwa? Sasa mnataka kuaribu hiyo mambo yenu? Kama ni mambo ya mashamba isipokuwa kuwe na kitu kipya kwa hivyo musiwemnarudia kila kitu unga mkono ama kama una kitu kipya uongeze kidogo umalize tunakubaliana hapo? Okay asante sasa-----tuliona hapa hakuna Charles M'tongania ni Samson M'tomungania kwa hivyo Samson ingia.

Samson M'tongania: Mimi naitwa M'tomungania. Nitaka Katiba hii ya sasa iondoe uvutaji wa bangi kwa maana hiyo bangi inaharibia jaama wengi sifa zao. Mimi namaliza.

Com. Ratanya: Okay asante sana hiyo bangi ni mbaya asante sana Samson Mungania. Sasa tuende kwa John Mundwa, nilisema kama hebu tuzikizana mwananchi nilisema kwamba ukiitwa kama uko hapa weka mkono juu. John Mwenda. John Mwenda hayuko. Joseph Kamayi huyo tumamaliza. Julius Ngolia, Julius Ngolia hayuko, Cyprian Ukunja? Justice Nguku? David Kamakia endelea.

David Kamakia: Asante sana. Maoni yangu ya kwanza--- kwa majina ni David Kamakia. Maoni yangu ni kwamba nataka hayamarekebisho ya Katiba, yaani Katiba ikitengenezwa kuwe kama ni Minister au DC au mtu yeyote Diplomat akipatikana na corruption, awe kwanza aondolewe kwa serikali, halafu apelekwe mahakamani na akitoka ashitakiwe kama shamba yake iuzwe.

Upande wa traffic: Katiba yetu tunaona watu kwa magari wanang'ang'ana kama ni Nissan inawekwa watu 30 sasa tunataka Katiba iwe kama na msimamo wa watu kama ni kumi na nane yule atapatikana akiweka access awe akichukuliwa hatua.

Ufisadi: Ufisadi unaenea hapa sana. Kama sisi tunaenda kwa office tukikuta kama ni askari ni lazima utoe kitu ili utengenezwe mambo kama unaenda kuchukuwa kitambulisho ni lazima utoe kitu kama unaenda kwa office unataka barua fulani ya mashamba ni lazima utoe kitu sasa tunataka Katiba iangaliye hiyo mambo na kuwe mtu akipatikana na ufiisadi ni hatua gani atachukuliwa. Vyama vingi: Kuwe kama ni (inaudible) ya KBC iwe ikishugulika na kama ni chama cha DP, KANU, NDP chochote kile kitakuwepo, wawe wanapewa masaa yanafanana. Kama ni chama upinziani inapewa masaa mbili kuongea na hii ya KANU inapewa masaa mbili na SDP siyo kuwa ati ni ili chama kinatawala inaongea tu. Sina mengine.

Com. Ratanya: Okay, tuende kwa huyu mwingine James Ngore, James hayuko? Samuel Imunya, Samuel Imunya? Isaiah Njoki? Isaiah Njoki? Gichugu Mngatia hakuna mkono ninaona kwa hivyo hayuko. Syllas Mutuma. Jacob Njoro, Sebestiano? Kimathi Syllas. Jeremia Kobia? Mwirigi. Francis M'tongai. John Meme? Isaac Muchugu? Francis Muchiri, Andrew Kobia? Julius Michugu? Ibrahim Michugu? Joseph Ngalu.

Joseph Ngalu: Asante sana Ma-commissioner kwa kufika kwetu hapa Laare. Mimi napendekeza ya kwamba Katiba mpya ijayo iweke mambo ya elimu kwanzia siyo ati kugawana gharama na serikali. Hiyo iondolewe. Mtoto awe akisoma kutoka standard one mpaka university kama nchi nyingine zile zinaendelea.

Hali ya afya ya mwananchi ilindwe kwa sababu gharama ya hospital siku hizi ni kubwa sana. Mtu awe hata akienda Kenyatta hospital alipiwe bill na serikali siyo kuuza mali yake.

Hatutaki kusikia nchi uhuru kama Kenya iko na ma-squota hiyo ma-squota ifikiriwe na itejengewe ardhi na serikali.

Mwananchi alindwe na mali yake. Asanteni.

(interjection) enda ukaandikishe jina pale.

Com. Ratanya: Jacabo Mwenda? Jacob Mwenda hayuko. Mkivicho Laiboni? Ni wewe okay.

Mukivicho Laiboni: Yangu itakuwa ni machache kuhusu ufukara au kumaliza umasikini. Majina yangu ni Zachearia Loiboni. Yale ningetaka kupendekeza katika Katiba mpya iwekwe ni upande wa kupunguza umasikini sisi wote hata pia Commissioners na wengine wote kama wazorora amani wa Kenya na wajumbe wetu wanajua pale umasikini inatuingilia sana mali tumelemewa na umasikini na hatutajua mpaka sasa ni michoro yetu ya barabara. Ningeomba Katiba mpya ipitishie sheria, barabara itachorwa mpya, maana yake sisi mtu akinunua gari, gari yetu humalizika na mwaka mmoja, na ya Mzungu ikiishi miaka kumi itakuwa imetembea kilometers ile yako inatembea mwaka moja. Kwa sababu hii --- sisi tukitoka Meru hapa tunapita Eastern Province, tunapita Central Province, tunapitia Rift Valley wakati tunafika upande wa Kajiado tukienda Mombasa, tunakuja tena mpaka Kitui ile tunapakana nayo. Hiyo nikuonyesha gari yako haiwezi kudumu kama ile ya mzungu maana yake barabara yetu imechorwa kwa urefu ihudumie Mzungu tu, yaani pale Mzungu alikuwa amelipa katika highlands ikawa ndiyo itapitia.

Com. Ratanya: Sasa unapendekeza nini?

Joseph: Yaani barabara zetu zichorwe upya, na Katiba mpya ikubali zichorwe upya. Sisi wa-Meru au watu wote ndani ya Kenya yaani serikali itoe sheria ya mila yetu ziendelee kama yule ametoa pesa ya kuendeleza waswahili Mombasa au wabaliya wamepewa pesa ya kuchukua mila yao. Mila yetu ichukuliwe sisi tukubaliwe kutengeneza ile nguo yenye tulikuwa tunaitwa kwa Kimeru nguo ya Muruku ndiyo wa-Meru wakienda huko kushona hiyo nguo awe na huyo kiongozi wao anaitwa Muruku na wawe wakishaurayana pamoja wawe wakitoa maoni pamoja ndiyo wawe wakilinda hata vijana yao na kujuana hao wenyewe ni wa-Meru.

Kitu ingine ningeongezea ni kuhusu Kilimo. Yaani serikali iweke kilimo number three kutoka Ministry ya education, kutoka Ministry ya health, kilimo kiwe ni cha tatu. Wawe (Inaudible) mambo kuhusu kilimo ndiyo watu wajiokoe. wakulima wapewe bank yao. Yaani kuwe na bank ya wakulima isiyo ambatana na zile zingine za serikali na isiwe na mawazo ya kiserikali.

Hii ingine kuomba ni makao ya wazee ianjishwe kote yaani katika Constituencies kuwe kuna makao ya wazee siyo huwa ukitunza watoto na mtu akizeeka naye awe hakuna mtu wakumtunza kuwe kuna makao ya wazee katika kila tarafa kwa hivyo hata wazee wataona kuna serikali ya kulinda kila mtu.

Mengine ningewaletea ni kuhusu survey yaani tumepewa mashamba katika minyanda za juu ambao kuna maporomoko na inaribu mazingira na wale (inaudible) yaani kunakuwa saa zingine ile mlima umepewa ndiyo hata --- mazingira ungepewa yaani

mashamba ya tambarari au serikali iongezewe kilimo ya maji ndiyo tusipewe milima au mabonde ya maji au chemichemi ya maji ndiyo tuchunge mazingira yetu sawasawa. Ni haya tu machache.

Com. Ratanya: Kamaru, Kamaru Joseph endelea.

Joseph Kamaru: Kwa majina yangu mimi naitwa Kamaru Josepha.Vile napendekeza ni kwamba katika hii election ya President the term should be reduced, ili awe anakaa term ya miaka tatu, and the Vice President awe anakuwa elected by the Members of the Parliament themselves. The Ministries should be reduced to a minimum of twelve, so that kuwe na ---- there is money in the economy so that we should not be claiming of jobs.

Na pale tunapo-elect our MPs tuliona ni lazima awe anakuja kuangalia watu wake at least kama siku ya Monday siku ya Wednesday na Saturday ili awe anatuambia ati yale tumempatia kama ameyapeleka huko. Pia ili tuwe tukimpatia shida zetu, halafu anatuambia vile tunaweza solve. Akiwa amezipeleka huko, anatuambia walisema nini siku ya Saturday, siku ya Alhamisi.

Tunaona hapo kwa land: kuwe na even distribution of land, kwa sababu tunaona pale kuna watu wale wakubwa wanachukuwa land ile kubwa.For us kuna watu ambao wana-suffer hata hawana mahali pa kukaa. Kwa hivyo napendekeza kwamba serikali ihakikishe kwamba kuna even distribution of land.

Na watu wale wafungwa wawe wanapewa ruhusa ya kuongea na watu wao kwa sababu kama wana kitu ambacho wangejizaidia nacho ama wangetaka kuzadiwa nacho ni vizuri kama wengepewa ruhusa waongea nao halafu wajadiliana ili waweze ku-set hiyo mambo kwa urahisi bila kukawia huko saana inaweza kufanya yule mtu akufe bila kufuata hiyo kesi ilikuwa imefanya ashikwe.

Kwa upande wa Miraa ningesema kwamba ati iwe protected na kuwe na ata external market ili tuwe tunauza hata huko nchi zingine kwa ushuru kidogo.

Kwa security: Ningetaka kusema kwamba serikali isitumie security wengi wale ambao ni mashujaa bila kuogopa wale watu wengine na wawe wanafanya kazi yao kwa uangalifu kwa sababu wakati mwingine tunaonanga wanakujanga kujifanya ati wanangalia shida zetu na wanaenda kujificha huku na tunakaguliwa na shida zetu.

Na kwa communication ningesama ya kwamba ile kama busta iko pale Nyambene iwe at least watu wa-meru tungetaka kuwe na kama satellite ingine iwe inatuletea zile habari zinazikika station zingine ili tuweze kuzungumza na ile ulimwengu ingine.

Kwa education ningesema kwamba hii education system ambayo inabadilishabadilisha na syllabuses ziwe zinabadilishwa kwa wakati ule unaofaa.Watu wanapewa mda ili ili kwa sababu ikibadilishwa kama leo wale walikuwa wanasoma saa ile unaona

sasa inawadhuru wale wengine walikuwa wanasoma hiyo system tunaona kwamba kama wale watu walikuwa wanasoma mpaka form six hawandangi tamacking sana kama sisi watu wa form four tunakaa kama hata hatukusoma. Asante.

Com. Ratanya: Gerald Ntonjira? Gerald?

Gerald Ntonjira Maroo: Mimi jina yangu ni Gerald Ntonyira Maroo. Kwa vile mimi ninasema Katiba nasema hivi. Serikali ichukuwe watu wakubwa kwa sahanati zote za serikali wasimamie wananchi maana yake wananchi wote huko sehemu za mashamba kwa wale wasiojeuza kwa maana awe na pesa ya kulipia pesa ya hospital. Sisi kuna wale wanajiweza na wale wasiojiweza.

Com. Ratanya: Unasemaje kwa wale wasiojiweza?

Gerald : Mimi ninasema serikali isimamie zahanati za serikali ziwe zikihudimia wananchi baadala ya kuhudumiwa kwa Private.

Serikali isimamia elimu maana yake watu wengi wanasoma elimu ya gumbaro lakini hawawezi hawataki kwenda shule maana yake ni wazee sasa hawa watoto tunazaa sisi badala ya kukaa bila kusoma serikali isimamia masomo iwe ndiyo inasimamia masomo watoto wote tunakaa wawe wakisoma.

Serikali isimamia habari ya mashamba maana yake ile watoto wanazaliwa na wazee iko watoto wanateswa na wazwe na wakitezwa wanakosa mashamba au wengine wataona mashamba na wazee wakauza mashamba watoto wanaachwa bila mashamba. Sina mengine.

Com. Ratanya: Jafeth Ngunja, kuja useme mafupi kabisa usirudie yale yote yamesemwa.

Japheth Ngunja: kwa majina naitwa Japheth Ngunja. Ningetaka kuchangia katika marekebisho wa Katiba juu ya elimu.

Ningeonelea ya kwamba elimu iwe haki ya kila mtoto anaye zaliwa katika nchi yetu ya Kenya kwa sababu katika Katiba ya sasa hayalindi watoto ambayo wanazaliwa kuna wale watoto ambao hawapati elimu kwa sababu wanatoka kwa jamii masikini.

Kwa hivyo ningeonelea ingekuwa ni bora Katiba yetu iwe ina angalia juu ya watoto wote watoto wale wanatoka kwa jamii masikini, watoto wale wanatoka kwa jamii ambayo iko na mali wote wawe wanajiriwa na serikali sawa.

Powers of the President should be minimized katika kuteuwa wale head of departments iwe ni kazi ya bunge. Bunge iwe na uwezo wa kuteuwa hawo department heads na ma-Judge wakuu kwa sababu hii uwezo wa President ndiyo unachangia corruption kushindi katika nchi yetu.

Kuna jambo lingine ambalo ningependa kupendekeza nalo ni early marriages.

Watoto wengi wasichana wanapoteza masomo yao kwa sababu ya kuolewa mapema. Unakuta mtoto ambaye yuko under 18 years ameolewa na yuko na watoto wawili ama watatu, kwa hivyo Katiba iangalie watoto hawaolewi bila kufikia umri wa miaka ishirini na kwenda juu. Kwa hivyo kwa hayo machache asante.

Com. Ratanya: Okay, asante sana. Tunaendelea kwa Justus Kiriamburi. Ni wewe Bwana, inua mkono. Ukiitwa hivi unainua mkono.

Justus Kiriamburi: Mimi naitwa Justus Kiriamburi. Nataka kusema ya kwamba Miraa yalalishwe kama mimea ingine kama Kahawa au Majini.

Nataka kusema ya kwamba Chief awe akichaguliwa na wananchi sababu anakwenda kuhudimia wananchi.

Ingingine nataka kusema ya kwamba elimu iwe ikisimamiwa na na serikali kutoka (inaudible) mpaka class ya juu. Sina nyingine. **Com. Ratanya:** Okay, asante sana. Luke Kaberia? Luke Kaberia yuko? Jacob

Jacob Mthiabiri: Majina yangu ni Jacob Thiabiri. Yala mambo nataka kuchangia katika Katiba kwa ile bidha inarundika katika nchi hii ni bidhaa zisizo za quality. Kwa hivyo napendekeza Katiba ilinde zile bidha zimeingizwa hapa kwa sababu zimekuwa za poor quality. Hata ukinunua haistahili hata ile pesa unanua nayo. Napendekeza irudishe ile price control ya bidhaa muhimu.

Nataka community iwe mobilized iwe inaweza ku-protect environment. Hapa kuna ile watu wanachaguliwa tuseme kama Rais watu wanapendekeza awe anatumika vipindi viwili napendekezo hivyo hivyo awe anatumika vipindi vya miaka tano tano ata wale MPs wawe wanatumika hivyo hivyo na Councillors wawe wanatumika hivyo hivyo.

Nonimation badala ya iongezwe, inatakiwa iwe ile ya 1997, na qualification ziendelea zile zile. Yaani hiyo ya language test iwe inatosha kumu-qualify mtu kuteuliwa. Wale wanateuliwa, I mean elected, kama Mayor ama Chairman wa Council wanatakiwa wafanyiwe election ya watu wote. Rais akiteuliwa ateuliwe pamoja na makamu wake siyo watu kuchagua makama yule anamuondoa wakati wowote ile anataka.

Kuna hawa Executive wengine badala watuliwe na mtu mmoja kuna ile special Commission wa kuwateu ama bunge. Nimeunga mikono wale wamesema Miraa isiwekwe kwa class ya dry iwekwe kama cash crop na ilindwe kwa vyovyote vile.

Kuna ile insecurity: Security inaendelea kupotea sana kila pahali kwa hivyo naomba Katiba iweke nguvu sana kwa security.

Kun hii vyama vya kisiasa, hii vyama vyetu vya kisiasa naomba Katiba ikubali viwe vinakuwa funded na public fund.

Tusema kama chama kimoja Kimeshinda kwa uchaguzi kuwe na coalition government ili vyama vyote viwe vinapata haki hiyo na sehemu zile ziko na upinzani pengine ziwe zinapata ile uhuru wa kuendelea na kazi zile za kawada. Kwa vile saa zimenda sana na mambo ingine imesemwa naachia hapo.

Com. Ratanya: Tuenda kwa Andrew Kaiga. Andrew Kaiga ni wewe? Okay endelea. Kama una memorandum hasa naona umebeba tuambia machache halafu peana hiyo.

Andrew Kaiga: Mimi nataka kusema maneno kidogo kwa sababu mengi yamesemwa, halafu nipeana hii report.

Com. Ratanya: Okay, dakika mbili.

Andrew Kaiga: Sawa sawa hata moja inatosha.

Kwa majina mimi ninaitwa Andrew Kaiga Munoru mimi ni Chairman wa Nyembene Miraa Train Association ambayo inaitwa Nyamita. Sasa (inaudible) tunasema an appeal itu-include and recognize Miraa as a major cash crop in Kenya.

Maneno mengine hapa yamesemwa kama vile Miraa. Tunaoa nayo vile tunapewa wakati tunaka kutairi watoto --- sasa hiyo yote sitarudia wacha – sababu Miraa iko na maneno kama number tano. Mimi nilikuwa nimeandika wacha niende number sita sasa.

Miraa is an important herbal medicine among the Wameru. It has been used for medicine curing heartburn, nusea---gonorea and depression. Its stimulating effect is good for delacation. Gankuuga miraa gwetu nituguraga iri ndawa jau jangi ni bugite, ni ndawa iritaga ngugi ya kirungurira, nithiragia kiinya nkoronjiru, ni nyomoo ithiragia gukora, nirijagwa niuntu bwa kiinya mpio taiji bugwita hasma na kiinya ngonoria miraa iri ndawa yayo mirii. Ningi still miraa ni iri ndawa ingi kiri ngombe, ngombe ikethirwa ikiaragwa ciongwa ukeja kumirugira miraa nirekaga kwarwaa kwou kiri ameru.

(Interjection) si utaongea Kimeru

Andrew Kaiga: Hapana, hawa wamejua nitakupatia hii, naambia hawa sababu wote hawasikii lugha ya Kiswahili tunayoongea.

Com. Ratanya: Andrew, lakini maaliza---

Andrew Kaiga: Yes, niko karibu kumaaliza si nilikuwa hiyo ndiyo ---.Sasa hapa kuna ma-resolutions tunataka tu kuongea hapa. When miraa is used without (inaudible) chemicals like drugs it still remain the very same plant, just like chewing of sweet gum or taboo chewed by the Indian community, miraa itibati kurujanirua na bingi, miraa itakunagwa yonka niuntu riria utakunaga utakunaga sitingamu kana uria wonaga aindi bagitakuna tabuu iria ciao naitibathukagia, kwou bugekira miraa mantu jangi.

Maneno mengine we are the Miraa farmers hereby status and believe that Miraa it is our cash crop and the government of Kenya should recognize and gazetted it together in the act that registers all the cash crops farmed and showed for the betterment of the Kenyan economy. Gatukuria turi arimi ba miraa atirii, thirikari ikire miraa sheryene iria ikirite kauwa na yakira bingi bira biendacua oome na biendacua Kenya biria tethecia nthii ii niuntu bwa utonga acia nimwe yayo. Miraa consumers should be informed not to (inaudible) with any chemical which shall be used for wound and --- changes. Gukeja kwithirwa wanywa bangi yaku, waeta kuria miraa niuntu antu bakuga noomiraa kiinya wakunda coobi yaku ukeja kuria miraa wija gukara ja miraa itumite ureba miraa tiu iethagia uu indi miraa itirijanagirua na bingi miraa irijagwa yonka na utibwo ithacia indi ka antu beenda gukira bungi tutikwenda buu miraa yetu nirijagwe na njira ya heshima.

We the farmers of Miraa are requesting the government, the new Constitution should enlist Miraa as a cash crop produced in Meru North District, commercially, although it grows --- in some other part of our country. Gatukuria thirikari iricognize miraa iri cash crop yetu ja antu ba Nyambene kiinya kethirwa niuma mwithune kungi niuntu ugeta gungu kungi ja Kerio Valley irikuo na kungi na kiinya Ethiopia irikuo kwou gwetu niyo minene thirikari nimenye niyo cash crop ya Nyambene. It is noted that Miraa is bought both locally and internationally and brings in foreign exchange. Apart from that, it improves the standard of living among the Wameru. Itwije miraa niyendagua oome na niretagira thirikari mbeba inyingi cia kigeni na still nituretagira mbeba itu tutura ukiene buu buri au kwou nibatikumenyekana. We farmers, we appeal the Ministry of agriculture to assist on the best way we can improve on the yield per plant. Gatukuria ministry of agriculture niuntu muti ni muti juri na maana nibashunguse batwone kiraa kii kibati kuandwa ruteere ruu kii gika ndwa kii gika andwa ruteere ruu kenda kiria giciaraga kilo jiji njira ii kiandwe kiandwe njira ee kigaciara kilo ithatu kana inya nibuo tukuria buu.. Thank you.

Com. Ratanya: Asante sana, saa hii nikwenda huyu mwingine anaitwa Vestus Muriungi. Vestus Muriungi. Peter Maore.

Peter Maore: My names are Peter Maore: I have this recommendations to be made in the Constitution we are going to have.

Our MPs should be accountable to the electorate, because once we elect our MPs they go to Nairobi and stay there forever, for four and a half years. They will stay in Nairobi only to come when the election is near. So the MPs should be accountable to the electorate.

The other thing Mr Commissioner Sir, our MPs should visit their Constituency every weekend, to hear the problems of the

electorate he should not stay in Nairobi alone.

The other thing is I would like to recommend that in the coming Constitution the MPs should not be allowed to increase their salaries as they want because the other workers have no pay because recently they increased their pay. The government should provide free education and health facilities to go (inaudible) this is our government should provide free education to every citizens from nursery schools to university because we pay taxes and it is the duty of the government to pay for these services.

The other thing is handling nursery school teachers should also be employed by the government. Nursery schools teachers those from the school and nursery school teachers should be employed by the government.

The forest act should be reviewed there are those individual who wants to destroy our Flora and Fauna for example our forest have been destroyed, have been grabbed by some people so the forest act should be amended so that those who are caught interfering with this forest because (inaudible) should be charged with a capital offence. Thank you.

Com. Ratanya: Sasa ni Mathia --- mwingine ni Gideon Muragwa.

Gideon Muragwa: Asante sana kwa kunipa nafasi hii. Okay yangu ni machache nataka kuomba serikali wakati Katiba inaenda kubadilishwa, kuwe na vyama vitatu tukipendekeza kwa sisi tukisema sisi ndio waundaji wa Katiba hii na kuwe vyama vichache kama vitatu kwenya Katiba hii.

Rais akichaguliwa awe ni kama anahitimu katika chuo kikuu.

Rais awe na umri wa miaka 45.

Rais anapaswa kuwa anapata asilimia 55 kwa kushinda kwa wingi wa kura. Tuna Donna wanatupa misaada kutoka nchi za nje na hawo donors wanatuletea misaada hii ya kusaidia kama wale watu wasiojiweza nauliza kwa Katiba hii ikiandikwa hivi sasa wawe ni kama siyo watu kupatiwa pesa hata kama pesa itaingia kwa tresurey ya serikali iwe inapasa kuwa ni kama zile zilikuwa za uhuru zinapewa watu na kushinda barabara za mashambani na zinatengeneza barabara na zinatengeneza milima ambaye inaleta mmonyoko wa udongo ili raia hawa wawe wakingia kwenye hizo kazi wakifanya kazi ya mashamba yao na wananzaidia kwa hiyo pesa kwa njia kupitia kazi hiyo ili isiwe ni pesa yakupewa watu iwe inazaidia hawa kwa njia hiyo ingine ya kuchimba mitaro wa mmonyoko wa udongo.

Naomba kwa Katiba hii ikiwekwa Assistance Chiefs hawana ma-camp ya kukutana na wananchi wanawakilisha wale wameajiriwa na serikali lakini ma-subchief ni watu manyumbani kwao hata raia wakitaka kuwaona hawampati kwa maana ni manyumbani mwao wako sasa naomba serikali ituzaidia ma-subchief hawa wanawandike wawe tukipata mahali wanaweza kukutania na wananchi ili waeleze maoni yao na shida zao zile wako nazo ili raia hawo wawezi kufaidika vizuri.

Serikali nahimiza upande wa security mahali wananchi watakuwa waki-report ma-report na kukutana na ma-subchiefs nahimiza kwa hii Katiba wawe wakitusikilia mzuri ili hii security iwe tukipata huduma za haraka kwa maaana tunapeleka huduma zinakawia zinamaliza siku mzima kama ni ng'ombe zinaenda zinaenda kabisa hatuna uzaidizi hapo tuwe tukizaidia serikali wakisikia tumetokea na mambao kama hayo wawe wakituzaidia na huduma za haraka ili tufaidike kupata vitu vinayoibiwa.

Yangu ni machache kwa hivyo kwa hayo machache ninasema asante sana.

Com. Ratanya: Sasa tuendelea na wengine lakini kwa sababu naona ya kwamba inaendelea kukuwa usiku kabisa tunataka kutumia njia ingine sasa nigetaka kuwaita wale ambao wako hapa wameandikwa kwa hii list tuona ni wangapi ili tujua kugawana masaa. Kama ni dakika tano tugawane kila mtu nusu dakika ili mtu aseme jambo asema kitu kidogo. Pengine mtu aweke mkono juu tuone kama yuko aseme yuko na tueke right tuone kama yuko.

Kariuki Karini, Julius Omolo, Muriuki, Ahmed Kabui, Severiko, Mtongoi, Lawrence Kithia, Peter Mito, Mito wapi hayuko, Mungania Mungathia, Joseph Kobia hata huyu hayuko? John Peter, Maritin Ntobutua, David Mugambi hayuko, M. Kinanga yuko, Julius Mwenda, Julius ulichelewa asubuhi. Ander Mwethi, Kiramburi, Joseph Kawaida, Kwa hivyo inaonekana tumemaliza na kwanzia sasa tutakuja kwa hao. Yes hebu hawa waje hapa wale ambao wameinua mkono, hata weka viti hapa hapa tu tuwe tunakuona tu. Wale walisikia majina na walikuwa wamejiandikisha wako hapa, walikuwa watu watano lakini hawo tumesoma sasa kama hukusikia kaa hapo. Sasa hawa ni watano na kila mmoja atakuwa na dakika mbili mbili. Ahmed Kabui, Ahmed Kabui?

Ahmed Kabui: Kwa majina mimi ni Ahmed Kabui. Kwa maoni yangu ama ningependekeza kutoa maoni yangu ni kwamba kuhusu Katiba tunayo na ile tunataka kuitengeneza. Katiba ambayo tunataka kutengeneza tunataka Katiba hiyo tuwe kama Rais anachaguliwa moja kwa moja na wananchi siyo kupitia kwa jimbo la bunge.

Pia tunataka Chiefs au sub-Chiefs wachaguliwe na wananchi.

Pia tunataka raia walindwe. Katiba ambayo tunaitarajia iwe inalinda wananchi kikamilivu, kwa vile inaonekana wakati huu Katiba tunayo inalinda tu wakubwa, siyo wananchi wale wanyonge. Inalinda tu wakubwa, ambao wengi ni watu wezi ambao hata wakiiba ng'ombe wanaenda nazo, ukiibiwa shamba inapotea hivyo hivyo; kwa hivyo tuwe na Katiba yenye wazi.

Pia ningependekeza upande wa dini: kwa vile dini pia ni haki yetu. Upande wa dini ya ki-Islam, napendekeza itambulike katika Katiba hii tunayoitengeneza. Kwa maana upande wa wa-Islam hawana siku kama wale wa-Kristo. Wa-Islam pia wapewe leave ikiwa ni Ijumaa waruhusiwe kwenda kwa ibaada zao, sio iwe unafanya kazi na ni siku yako ya maombi. Lazima kuwe na uhuru huo katika Katiba hii tunayoitengeneza.

Pia tunaomba watu kama Mayor wenye kiti ambaye za Ulaya pia nawo wachaguliwe. Kwa hivyo asante.

Com. Ratanya: Sasa tuenda kwa Lawrence Kithia.

Lawrence Kithia: Jina langu ni Lawrence Kithia na nashukuru sana kwa kuletewa hii Katiba hapa mwisho. Mambo yangu ni matatu tu nitaongea.

Nitaongea upande wa mwananchi wa kawaida, hana huruma kabisa. Kwa sababu tunaona hii Katiba ifinye kabisa, hii Katiba ya ku-mwananchi wa kawaida, akiwa mwingine akisha kufa kabla hata machozi yajakwisha kwa macho ya mwenye, huyo mtu mara moja tunaona huyo mtu hata hajafanyiwa hata kitu. Mbeleni tulikuwa tunaona mwananchi wa kawaida akiua mwingine hata rumandi anawekwa kwa rumande apate bond. Lakini siku hizi hata bila machozi kukwisha kwa macho ya wenye kuuwiwa yule mtu tunaona yule mtu amekuja.

Sisi tuna mwananchi wa kawaida; tunasikia kuna majangili, wanachukua ng'ombe. Tunasikia ng'ombe zimechukuliwa hapa kama ng'ombe mia moja, na zimeenda. Tunaona serikali ni wengi sana. Ng'ombe ikienda pale ukifuata unapata barabara kubwa lakini tukisikia sisi kwa Serikali yetu zile ng'ombe hazipatikani. Sisi wananchi wenyewe ndio tunanunua ndege, tunanunua kila kitu. Serikali ni yetu, lakini tukienda tunaambiwa ngojeni mukatafute ng'ombe hiyo. Katiba iwekwe mkazo kabisa. Ikiwekwa mkazo pale ng'ombe inapitia, mpaka pahali itapatikana mmoja hawa watu ---- sababu hii wizi wa majangili umekuwa mwingi sana, na umekuwa ukisumbua mwananchi.

Ukisha enda mashambani uko unakwenda kukuta watu wakilima shamba hata akina mama wasichana wa watu wanaokotwa na Serikali wanajaa hapa wanaandikwa. Ndiyo naomba Katiba kabisa ifinye hicho kitu mwananchi wa kawaida hata kama unamchangia elfu mia moja hakuna kitu umeaaidia.

Tufungiwe kutoka huku mpaka swariri ya ndani, halafu tujue mwananchi wa kawaida ametawala. Ni hayo tu sina mengine.

Com. Ratanya: Asante sana. Kuna Peter? John Peter.

John Peter: Kwa majina ninaitwa John Peter Kihoria. Mambo yale ningependa kuzungumzia ni mambo machache kwa sababu mengi yamezunguzwa. Jambo la kwanza ningezungumzia kuhusu the National cake. It should be shared by everybody kwa sababu kila mwananchi wakati huu inaonekana ya kwamba chochote mtu ananunua ushuru anakata. Kwa hivyo ni vizuri mwananchi yeyote awe ana-share katika National cake.

Jambo lingine ni kuhusu watu wale wote wamesoma. Kama mtu amesoma ako na right ya kuwa ameajiriwa na Serikali. Ukianda Serikali za ng'ambo utakuta ya kwamba kila mtu analipwa kwa sababu amesoma na kila mtu Serikali inajua ya

kwamba kila mtu anapata share kidogo kutokana na zile peza inapatikana. Unakuta Kenya wakati budget inasomwa unasikia ya kwamba kila mwananchi anahesabiwa peza zake ikiwa ni 70 shillings, lakini yule mwananchi wa kawaida afikiwe na ile pesa kwa sababu there are some people wale wako juu ndiyo wana-take the whole amount. Kwa hivyo jambo lile ningenelea katika nchi yetu ni vizuri kila mwananchi ama mtu yule amesoma, tuseme kutengenezwa a system ya kwamba huyo mtu ni lazima aajariwe. Kama vile watu wamesema mambo mengi kuhusu Rais awe na tenure mbili au miaka mitano mitano mara mbili, naye kila civil servant anatakiwa hata yeye awe hivyo kwa sababu kila mtu ako na right to ku-share this National cake.

Jambo lingine lile ningepanda kusema ni kuhusu the Cabinet ya Kenya, ya kwamba Rais amepatiwa huo uwezo wote. Kwa hivyo anaweza kuku-appoint today na akienda njiani unasikia kwamba amekufuta kazi kwa hivyo jambo lile liko mzuri hapo ni ya kwamba Cabinet yetu ile mtu asikiaye kwamba ako na uwezo na aweze kusimamia ile kazi vizuri bila kuogopa ni vizuri awe akichaguliwa na Parliament. Kwa hivyo Parliament ipatiwe uwezo wote.

Na kama vile wengine wengi wamesema hapa mbeleni sitarudia kuhusu Chief justice na Attorney General, wachaguliwe na Parliament, hiyo ningeeunga mkono.

Halafu District zile ziko katika Kenya ni nyingi sana ya kwamba tuko na DCs wengi na DC anataka watu wakumtumikia. Kwa hivyo tunaona ya kwamba kila wakati kunaongezwa District kila wakati kunaongezwa kwa hivyo District kwa maoni yangu mimi ningeeona katika Constitution mpya na District guaranteed katika Kenya na Constituencies nazo ziwe minimized ili economy ya Kenya iwe mzuri kwa hivyo iwe Constituencies 150.

Katika Ministries tuwe na Ministries 12 na Assistance Ministers wawe assistance 24.

Vice President: Ni vizuri Vice President wa Kenya awe anachaguliwa na Parliament kwa sababu unakuta ya kwamba Kenya wakati mmoja tulikaa one and a half years bila Vice President na jambo hilo lilikuwa mbaya sana kwa sababu President jambo lolote lingetokea kwake hatungekuwa na President yule angekalia kiti for 90 days. Kwa hivyo kwa hayo machache ninasema ni asante na Mungu awabariki.

Com. Ratanya: Okay asante sana Bwana Peter---. Julius Mwenda.

yale mambo mimi nakuja kuongeza ni ile ilikuwa ya Miraa hata ile result nilikuwa nayo ilikuwa ya kusema Miraa. Ni kitu muhimu badhi ya kwetu kwa sababu sisi hiyo ni kitu ile mungu ametupa sisi Serikali iangalia sawa sawa. Hata wakitaka kutuma watu huko ndani ya mashamba wakute wenye mashamba wakute wajue Miraa ni kitu kizuri. Na mimi ninasema Serikali ituangalie ituongoze hata mahali ya kuuza hii kitu chetu badhi ya nje. Asante.

Com. Ratanya: M. Kinanga.

M. Kinanga: Jina langu naitwa M. Kinanga. Nataka kusema tukifanya hiyo mambo ya Katiba mimi ninasema Rais ndiye controllowe ndiye anaweza controller watu wake wote vile mwenyewe anataka. Hapa Kenya sisi tunaumia sana kwa vitabu, kwa kununua vitabu ya watoto wa shule na wakati Mzee Hayati Jomo Kenyatta alikuweco tulikuwa tunapata vitabu ya kusoma mzuri sana.

Na jambo lingine lile mimi ninasema kwa hii Katiba hata hospital, ukienda hospital ya privat unapata dawa, lakini ya Serikali hakuna dawa unaweza pata.

Ile jambo lingine nasema kwa hii Katiba yetu ni kuhusu kama ni magari, hongo iishe, kama ni abiria ndiyo wananinginia kwa gari si wanambia ati waingie kwa nguvu hawa ndiyo wanatakiwa wastakiwe kwa sababu hawa ndio wanaingia kwa gari ikiwa hata inajaa watu.

Mambo mengine yale mimi nataka kusema ya Katiba ni ya waalimu. Kwa sababu mwalimu anafanya kazi ngumu sana ya kusomesha mtoto, hata anasomesha mtoto asiye na macho na anajua kuandika. Sasa hiyo ndiyo Katiba mimi nataka ipinduliwe hapa Kenya yetu. Asante sana.

Com. Ratanya: Sasa ati wewe unasema ulikuwa umeandikwa. Sasa wananchi --- kumekuwa karibu kabisa saa yetu ata imebakishwa kidogo dakika kama ishirini hivi. Sasa tungetaka kuona wale ambao --- unajua kuna watu ambao wanakuja sasa hivi na wengine walikuja saa mbili, kwa hivyo mtu wakuja jioni huyo alichelewa. Lakini wale waliitwa lakini wakakosa hebu mkono juu tuone mikono juu. Mikono juu, na hawa ndiyo wanataka kusema kitu. Excuse me hata wengine kwa sababu tutaomba mketi tu, tuwe tunaomba pamoja kwa sababu tunaenda sasa. Sasa wale wanataka kuongea ni hawa. Wale wanataka kuongea, keti mzee, keti tu keti, kwanza keti hapo.

Kuna mwingine anataka kuongea hapo. Sasa hawa pengine hawa ni observers. Wengine nyinyi mmetosheka ni sawa sawa, munangoja tuombe pamoja. Sasa hawa ndio wanazungumza yule mzee zaidi ya wengine wote.

Mugambi Mulu: Jina langu naitwa Mugambi Muli:

Basi kina kitu kimoja mimi ninauliza.

Mimi ni Mukunga wa kienyeji ninajua kutengeneza zile dawa zile za kienyeji naomba Katiba yetu itupatie pesa za kutengeneza zile dawa zetu za kienyeji maana tunakosa nini nguvu za kufanya hizo dawa zetu.

Ingingine ni kitu ambaye mimi naomba kwa serikali yetu tukufu kuna ndugu wako alipochukuwa shamba lako na akiwa alichukuwa alichukuwa tittle na shamba hilo lako ulikuwa umeandikiwa na number yako na akawaga dunia akakuwacha na shamba lile lako. Ndugu wako akapima wakati alipopima, ukimuuliza anakuambia mimi nina tittle, nataka serikali yetu tukufu ichunguze

title kwa sababu ndiyo zaidi ya mzazi.

Com. Ratanya: Umemaliza sasa.

Mugambi Muli: Kunaye njia nyingine nayo maskini wale hawana pesa wananyang'anywa mashamba yao kwa kuwa hawana pesa. Unanyang'anywa shamba, ukienda kusema unaambiwa hakuna shamba lako liliondoka. Basi naomba Serikali yetu tukufu wakati itakayo kubadilisha Katiba, ibadilishe ikijua maskini ndiyo wengi kuliko watajiri.

Com. Ratanya: Sebastian Kimathi. Sema jina lako haraka.

Sebastian Kimathi: I am Sebastian Kimathi Isaac. I have two points.

First point is about the employment: For all Kenyans to have equal chances of enjoying cake I propose that in all areas of jobs where there is --- let all those who have the same profession be divided into groups whereby first group can serve for a specified period of time lets say two years and then the second group can serve the same period.

No there is no need for government to terminate some colleges from progressing for sometime. Really if the same Kenyans have used the same resources to get the same profession let them also be given equal chances to gain out of their profession.

Polical engineering: All politicians should be holders of degrees, Diplomas or certificate in Political engineering. I propose this so that we may have competent and confident leaders to quard our nation effectively. This will avoid double involvement of leaders in various business. e.g somebody being a doctor should not become an MP nor a teacher become an MP. This is because some being a doctor can decide to run a clinic, while he is serving as MP, hence paralyzing the service of being an MP and this is whereby you see someone if he is in Parliament, anaingia tuna that door, anatoka na hiyo door, and he goes to another business.

Com. Ratanya: (inaudible)

Sebastian Kimathi: Also I propose that when the President appoint a certain Commission and after sometime he nullify that Commission he should be held responsible of all the expenses which have been used by that Commission. Thank you.

Com. Ratanya: Asante sana. Endelea.

M'tomuchiri Kaimwenwa: Mimi kwa jina naitwa M'ntomuchiri Kairmwendwa niliandikwa pale asubuhi.

Yale mazito ni machache. Serikali yetu ya Kenya Katiba yetu ikibalishwa kwa maoni yangu naona mtu au vikundi vipewe

katika Mikoa yetu yote ikiwa ni maji ikiwa taaba ni ya maaji vikundi vinafaa kupewa nafasi wakachimbe maji yao mahali watapata.

Maskini haina mwenyewe siku hizi. Kila Mikoa ina mahali yao na sisi hapa kwetu Ntonyiri hatuna ulinzi wowote hakuna security. Kwa haya yangu machache ni hayo.

Com. Ratanya: Asante sana. Tunaenda kwa mwingine.

Francis Muturia: Jina ni Francis Muturia Kwa maoni yangu kuhusu Katiba yetu mpya, sitarudia sana yale ya Miraa yamesemwa lakini wale wote wamesema mambo ya Miraa nawaunga mkono. Nikisema Miraa ni rasilimali yetu, ndiyo tunaoa nayo, ndiyo tunasomeshwa nayo watoto, na Miraa iwekwe umuhimu sana katika Katiba.

Mambo ya shule: hapo zamani tulikuwa tunapewa kule shuleni vitabu, na ile ingine kiti cha kupaguza number kama rubber, na kalamu; lakini siku hizi zimepotea. Ndani ya Katiba yetu mpya hiyo irudi tena.

Yale nikimalizia kabisa, ni kuhusu mambo ya kilimo. Mambo ya kilimo: Katiba yetu mpya ishirikishe kilimo, watu wafanye makundi ile tuweze kuweka nafaka yetu vizuri. Katiba ilinde bila kuuzia watu huko mashambani huko ndani kule, ili kwa kuchukuwa vitu vyetu halafu wakaenda kuuza, kama vile Kahawa wanasema wanafanya siku hizi. Kahawa kuna watu wengine wanajifanya kama manager wa Kahawa huko ndani, wanachukuwa Kahawa ya wananchi, wanauziwa kule, wakapeleka factory kwa njia yao wenyewe wakafaidika, na sisi tukakonda kwa sababu----

Com. Ratanya: Sasa unapendekeza nini?

Francis Mururia: Sasa napendekeza serikali isimamie wale wanachukuwa licence ya kununua kule ma-shambani waache. Kwa hayo machache asante.

Com. Ratanya: (inaudible)

Kanuru Mithika: Jina langu ni Kanuru Mithika. Ya kwanza nitaongea kuhusu mambo ya Katiba. Kwanza upande wa hii area ya Ntonyiri hata Mtukufu Rais akiongea maneno ya kuhusu zile pesa ya activity fees kila wakati mwalimu Mkuu watoto wetu wanasumbuliwa kuonekana barabarani ----wamesoma half day.

Com. Ratanya: Pendekeza

Kanunuru Mithika: Hiyo -----

Com. Zein: Ndugu yangu sisi ni ma-Commissioner tunapendekeze tu----- hadithi ---**Kanuru Mithika:** Nitaongea kuhusu

Administration Police ile (inaudible) Bwana Commissioner ukiambiwa ati ilimaliza mashamba. Copral akipigwa transfer kituo Fulani, naye analemea, anachukua misaada double, mbili kila one week. One thousand analipa na wale wamepika ile pombe ya haramu, hongo iishe.

Ya tatu nitaongeza wazee wa Njuricheke waweke katika laini ya mawakili kulingana na vile mutapanga arrangement yenu. Hata mtu akikodishia mwingine Miraa ama kumuzia mashamba bila agreement, sababu inaweza ----- at night ukaenda ukakimbia kwa mwenzako ukachukuwa elfu tano, umemuruka kortini halafu ukirudi hapa kwa wazee wa Njuricheke, wanakubali. Asanteni.

Com. Ratanya: Andika jina pale kwenya register.

Festus Kanyanu: Mimi naitwa Festus Kanyanu na mimi nataka kuchangia hii Katiba mpya ya Kenya, maana ndiyo itatulinda.

Nataka serikali ifikirie kuhusu wale ambao ni wanyonge, iwaelekeze katika mradi wowote. Tena iwe katika ma-office yetu ya serikali iwe haina ubaguzi, maana unaweza kwenda hapa kwa police ukipiga report kama una chochote kile unatupwa ikawa wewe hushugulikiwi, ukawa kama wewe si raia. Ukifanywa jambo na mtu unanyamaza, ukachukua hatua ya kuamungamiza maana hakuna sheria ya kusimamia wewe, kama hauna chochote.

Ya mwisho: ningetaka yaani kama ni rasilimali ya Kenya, iwe ikigawiwa wa-Kenya kwa jumla. Raia wa Kenya nao waishi mahali popote pasipo ubaguzi wowote. Katika Katiba yetu iwe raia wa Kenya anakaa mahali anataka bila kubagaliwa na bila kuambiwa ni mbara au ni mtu wa kabila gani. Aishi mahali popote katika Kenya.

Com. Ratanya: Mwingine.

Paul Mathindi: Jina langu naitwa Paul Matindi. Napendekeza Katiba yetu ya Kenya mwaka huu tunaenda tuwe hakuna corruption. Tuwe na sub-Chiefs wa kutosha. Tukimaliza hizo zote hata wa raia wale wachanga wale wanyonge, watafaidika na hawatakuwa wezi.

Tukiwa na security ya kutosha hakuna yule mtu atawawa akose mtu kupata yule mtu anaua mwingine. Hata wale viongozi wetu wengine wafisadi wawe wakipewa nafasi ya kuongea vizuri.

Com. Ratanya: Na mwingine.

Bunge Mungathia: Jina langu naitwa Bunge Mungathia: Thank you Bwana Commissioner mimi napenda kuongea nikiwa nasimama. Yangu yale mimi ningetaka kusema, nitasema mambo tatu. Katika Katiba ya Kenya, ikienda kuangaliwa vile itapendekeza---- Akiwa hawafanyii kazi, wale wanaenda na wana-report. Sababu tunachagua wajumbe wanaenda Nairobi na

sisi hatujui wanaenda kufanya nini Nairobi.

Ya pili Commissioner ningetaka kusema hivi Katiba yetu, Chiefs au sub-Chiefs wachaguliwe kwa kura.

Ya tatu Bwana Commissioner, mimi ningesema haya maneno yote yamezungumzwa hapa sitarudia, maneno ya Miraa Miraa, sitarudia.

Com. Ratanya: Micheal Koome.

Michael Koome: Asante Bwana Commissioner kwa majina mimi naitwa Micheal Koome. Kwenya haya marekebisho ya Katiba hii nataka kuchangia mambo mawili.

Jambo la kwanza ni jambo ambalo linahusu kitambulisho. Unapoenda kwa hao ma-officer ambao wanahusika naupeanaji wa vitambulisho, unambiwa ati nende ulete kitambulisho cha mama yako au baba yako (inaudible). Sasa na hapo pengine unaweza kuwa ulizaliwa kuwa chokora ata hujui mama yako. Sasa ningependekeza hivi, Chief ndiye ako karibu na mwananchi na ndiye anamuelewa vizuri. Chiefu apewe uwezo kutambulisha huyu mwananchi.

Jambo la pili ni juu ya waalimu: Mwalimu kwa kweli anafanya kazi ya maana. Katika hii Katiba tunarekebisha wakati huu, iangalie mambo ya mwalimu vizuri, na apewe mshahara mkubwa. Angalia kama hawa wabunge, ile mishahara yao inaweza katwa ikaongezewa waalimu ndiyo kuepukana ni hizi migomo migomo ya kila wakati. Asante Bwana Commissioner.

Com. Ratanya: Okay, asante sana. (inaudible)

Jacob Nchunga: Ntiji kwaria githwairi ni tabutirwe. Mbitagwa Jacob Mnkubitu wa Kiunga.

Translator: My name is Jacob Nchunga.

Jacob Nchunga: Uuni buu kuga nikakuga indi buumbona au ndina miaka mirongo mugwanja na kethrwa tii miraa

Translator: I am 70 years old, and were it not for Miraa

Jacob Nchunga: kethirwa tii miraa ntikithirwa nkari uu bumwe bunene ndina jontu nandi baruga ii ngwete aa ndina antu bairi secondary.

Translator: I want to emphasize the importance of Miraa in this place it has maintained even my children in school.

Jacob Nchunga: Nindiina umwe form four Mikinduri ungi Kangeta.

Translator: Through the money that I get from Miraa, I have been able to support my family I have children in high school.

Jacob Nchunga: Gutiri mwana umbikiraga baaba bangi akuru.

Translator: It is only through Miraa that I get this money .

Jacob Nchunga: Itu nika nkwerenka katiba thirikari ya Kenya itu nitethie akuru ba Ntonyiri na Igembe na kwanja North Nyambene.

Translator: I am now suggesting that the new Constitution that we are coming up with should be put into consideration the issue of Miraa and a provision for it must be there.

Jacob Nchungu: Uuni buu nkuga au nika nkuuga thirikari ya Kenya nioririe yone batwi jontu naa turi mwankene jwa Borona batwii turi ameru baria bamuthia guti antu bathoma naa bangi nibatwi tweja kuthomihtia aana.

Translator: We want to put it that we border the last part of this Nyambene district, and the issue of security is very important for us.

Jacob Nchungu: miraa iu ndikomborithia muntu eja agankana, eja ankana kethirwa batwi niungu kuuga gatiba niorerue bwega nkethirwa ndi wa Kobia ngeeta kiri Kobia kethirwa ndi wa Kaberia ngeeta gwake. Nandi ngeeta kiri njuri niyo intethagia.

Translator: So I am still emphasizing on the issue of Miraa,.It should be given a provision in the Constitution.

If I go to local elders organization, I get some help there. Thank you.

Com. Ratanya: The Chairman of 3Cs. Chairman yuko wapi?

Chairman sasa utasema machache halafu uombe na tufunge.

Julius Kaithuru: Let me say, thank you very much to our commissioners for having availed themselves throughtout the day so as to hear our views. May God bless you. May I also thank those who have given their views, for having found time to come and help in preparing the Kenya Constitution. Thank you.

Com. Ratanya: Una kitu cha kusema halafu tuombe? Okey, kwa hivyo tuone mtu wa kutufungia kwa maombi. Ningetaka kusema asante sana kwa wale wote tumekuwa nao, wananchi ambao wamepeana maoni yao, na wale ambao wamekuwa wakitayarisha hiki kikao kama Chairman, Coordinator, na wengine wote ambao wanamsaidia, tumesema asante kwa --- watu wa Laari. Kesho wale ambao hawakupeana maoni hapa, lakini hakuna kwa sababu tumemaliza,tutaenda upande wa Mtuati. Tungali tuko katika Ntonyiri, na kwa hivyo tumemaliza na tumefunga kikao hiki cha Constitution of Kenya Review Commission. Lakini tuombewe.

Julius Kaithuru: Let us pray: Father in the name of Jesus, we are in your presence this particular time. We thank you for giving us an opportunity to have a wonderful forum like this one.We thank you for it.We thank you because, Lord, we have

